منهاج المسلم - سواحيلي

# UTARATIBU WA MUISLAMU



جمعية الدعوة بالزلفي


جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# UTARATIBU WA MUISLAMU

## منهاج المسلم - سواحيلي

Kitafsiriwa na kupitiwa na:
Al Akh: Ally Nassoro Ally
Al Akh: Mwichande Mohamed Ally


جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
Tel: 966 164234466 - Fax: 966 164234477

بسم الله الرحمن الرحيم

منهاج المسلم

# KUMUAMINI ALLAH:

Muislamu anamuamini Allah Mtukufu, kwa maana ya kuwa anakubali uwepo wa Mola mlezi - utakasifu ni wake-, na kwamba yeye Mtukufu, ndiye muumba wa mbingu na ardhi, anajua vilivyojificha, na vinavyo onekana. Ni Mola Mlezi wa kila kitu na mmiliki wake. Hapana anayepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye tu, na kwamba yeye Allah -utakatifu ni wake- ana sifa zote za ukamilifu, ame epuka na kila aina ya dosari (upungufu) hayo ni kwa mujibu wa dalili za kunakili na za kiakili, miongini mwa dalili hizi:

Ya kwanza: ni kujielezea Allah mtukufu yeye mwenyewe kuhusu kuwepo kwake na uumbaji wake viumbe, na kuhusu majina yake na sifa zake na katika hizo ni kauli yake Mtukufu:
(Hakika Mola wenu Mlezi ni Allah Aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha akawa

juu ya Arsh, huufunika usiku kwa mchana, huutafuta mno. Na jua, mwezi na nyote vimetiishwa kwa amri yake. Elewa ni juu yake tu suala la kuumba na kuamuru, ametukuka Allah, bwana wa viumbe wote. [54.Al Araaf].
Na kauli yake:

(Kwa hakika mimi ndiye Allah, hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa mimi, basi niabudu mimi, na simamisha swala kwa ajili ya kunikumbuka.)[1] [twaha,14].

**Na kauli yake:** (Lau ingekuwa katika mbingu na ardhi kuna Miungu wengi (kila mmoja anapanga lake)bila shaka zinge haribika, basi ametakasika Allah Bwana wa Arshi na yote wanayo msingizia.) [2]

Basi pia kuwepo nyenzo hizi tofauti tofauti, na viumbe mbali mbali ni ushahidi juu ya kuwepo muumba wake, naye ni Allah Mtukufu.pale ilipokuwa katika uwepo huu hakuna aliye dai kuumba viumbe hawa na kuvifanya viwepo, kama ilivyo kwa akili ya kiumbe kwamba

---

[1] Sura Twaha (20) Aya ya 14
[2] Sura Al ambiyaa (21) Aya ya 22

haikubali kuwepo kwa kitu bila ya aliyekifanya kiwepo. Na kwa mfano wa dalili hizi za kiakili na za maandiko na nyinginezo, Muislamu amemuamini Allah Mtukufu na uumbaji wake wa kila kitu, na Uungu wake ni kwa wa mwanzo na wa mwisho.

Ya pili: upweke wake katika kutoa riziki, kuwa yeye Allah ni pekee mwenye kutoa riziki kwa viume wake wote, Allah anasema: (Na hakuna chochote kitembeacho ardhini isipokuwa ni juu ya Allah kukiruzuku,...).[3]

**Ya tatu**: Ushahidi wa maumbile ya kibinadamu yaliyo salama ya kuwa mola mlezi wake ni ya Allah mtukufu, bila shaka kila mwanadamu anahisi hilo katika dhati ya nafsi yake. Allah anasema: (Sema hivi ni nani Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa Arshi iliyo kubwa? Watasema ni ya Allah,...) [4].

---

[3] Sura Hudi (11) Aya ya 6

[4] Sura Muumununa (23) Aya ya 86-87.

**Ya nne**: upweke wake katika ufalme wa kila kitu, na kuwa yeye ndiye mwendeshaji wa mambo yote, na hana mipaka:
Allah anasema: (Sema, hivi, ni nani anaye waruzukuni mbinguni na ardhini, au ni nani anayemiliki kusikia na kuona, na ni nani anayemtoa aliye hai kutoka katika maiti, na anamtoa maiti kutoka kwenye uhai, na ni nani anayendesha mambo basi watasema, ni Allah, basi waambie hivi kwa nini hamumuogopi. Na huyo kwenu ndiye Allah bwana wenu wa haki, na hakuna baada ya haki isipokuwa ni upotevu tu?...)[5]

Na pia Muislamu anaamini Uungu wa Allah kwa wote, Na hakuna wa kuabudiwa kwa haki zaidi yake, Allah anasema: (Allah ameshuhudia kuwa hakuna wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye, na Malaika (pia wameshuhudia) na wenye elimu, kuwa amesimamia usawa, hakuna wa kuabudiwa isipokuwa yeye, Mwenye nguvu sana Mwenye hekima mno."[6]

---

[5] Sura Yunus (10) Aya ya 31-32
[6] Sura Aali imran (3) Aya ya 18

Na kauli yake Allah: (Na mola wenu mlezi ni mola mmoja pekee, hakuna wa kuabudiwa isipokuwa yeye, Mwenye rehema Mwenye kurehemu mno).7

Na miongoni mwa dalili za Allah Mtukufu zinazothibitisha kuwa yeye tu ndiye anaye stahiki kuabudiwa, ni habari walizotoa Mitume yake – Amani ya Allah iwe juu yao-, na ulinganizi wao kwa watu wao, wa kumuabudu yeye Allah pekee, na hakika Mtume Nuhu amesema: (Enyi watu wangu, muabuduni Allah hamna nyinyi Mungu mwingine asiye kuwa yeye, hakika mimi naogopa kwenu kuwapata adhabu ya Siku kubwa.[8]

Na vivyo hivyo alisema Nabii Hudi: (Hamna nyinyi Mungu mwingine asiye kuwa yeye[9]

Na Allah amesema: (Na kwa hakika tulipeleka katika kila umma Mtume (akiwaambia) Muabuduni Allah na jiepusheni na twaghuti)[10]

---

[7] Sura Al baqara (2) Aya ya 163.
[8] Sura Al araafi (7) Aya ya 59
[9] Al aarafi (7) Aya ya 73

TWAGHUTI: ni kila kinacho abudiwa kinyume na Allah.

Na anasema Mtume Allah - Rehema na amani zimfikie- kumwambia Abdillahi bin Abbas- radhi za Allah ziwe juu yao, ya kuwa:
(Ewe kijana hakika mimi ninakufundisha maneno: Muhifadhi Allah atakuhifadhi, muhifadhi Allah utamkuta mbele yako. Pindi unapo omba, muombe Allah na utakapo msaada basi taka msaada kwa Allah, na elewa ya kwamba hata umma ukikusanyika kwa lengo la kukunufaisha kwa jambo, kamwe hawataweza kukupa manufaa kwa chochote isipokuwa kwa kitu ambacho Allah alishakuandikia ukipate. Na endapo watakusanyika kwa lengo la kukudhuru kwa jambo kamwe hawatakudhuru kwa chochote isipokuwa kwa kitu alichokuandikia Allah kikupate. Kalamu zimeshanyanyuka (kuandika hayo) na (maandiko) yameshakauka.[11]

[10] Sura Annahli (16) Aya ya 36.
[11] Sahihi Atirmidhy 2516

**Na kauli yake** Mtume - Rehema na amani zimfikie- aliposema: (Na kwa hakika hakutakwi msaada kwangu. Hakika si vingine anayeombwa msaada ni Allah pekee).[12]

**Na kauli yake** - Rehema na amani zimfikie-: (yeyote atakaye apa kwa asiye kuwa Allah kwa hakika amemshirikisha Allah).[13]

**Na kauli yake Mtume** -Allah amshushie rehema na amani- (Hakika Ruqyah (matabano) na Tamaymu (hirizi) ni ushirikishaji).[14]

Pia Muislamu anaamini yale majina na sifa mzuri za Allah Mtukufu, na hamshirikishi asiye kuwa Allah Mtukufu nayo, na hazitafsiri kinyume, na hazipi maana nyingine isiyo yake, na hazishabihishi na sifa za viumbe, bali tu anathibitisha kile alichokithibitisha Allah mwenyewe na kile alichokithibitisha Mtume wake -Allah amshushie rehema na amani- katika majina na sifa. Na anakana kwa Allah

[12] Hadithi hii imenukuliwa na Atwabarany katika kaulu almufid 277
[13] Hadithi imenukuliwa na imamu Atirmidhy
[14] Hadithi imenukuliwa na Imammu Ahmad 1/381.

kila kile alichokikana mwenyewe, na amekikana Mtume wake miongoni mwa kila aibu na upungufu, Allah amesema: (Na Allah Mtukufu ana majina mazuri (yanayo julisha utukufu wake) basi muombeni kupitia majina hayo, na waacheni wale wanaokaidi katika majina yake, watalipwa yale waliyokuwa wakiyafanya[15]

**Na kauli yake Allah**: (Sema ombeni kwa kutumia jina Allah au Alrahmani, lolote mtakalotumia kuomba, basi yeye ana majina mazuri...[16]

Pia miongoni mwa dalili, ni habari alizotoa Mtume wake- Allah amshushie rehema na amani- , kuhusu hilo kama aliposema:
(Allah anawachekea watu wawili, mmoja wao anamuua mwingine , wote wanaingia peponi.[17]

**Na kauli yake Mtume** - Rehema na amani zimfikie-: (Jehannamu itaendelea kutupwa humo (waasi), nayo itasema: Je kuna ziada?

[15] Sura Al araafi (7) Aya ya 180
[16] Sura Al israa (17) Aya ya 110
[17] Hadithi imenukuliwa na Imamu Bukhary na Imamu Muslim

Hadi atakapoweka Allah mguu wake-na katika mapokezi mengine- unyayo wake, basi hapo utajisongana songana wenyewe na kusema hii inanitosha)."[18]

Na Muislamu pale anapo amini sifa za Allah Mtukufu, na akamsifu kwa sifa hizo, kamwe hato amini na kuitakidi wala kufikiria kwenye akili yake kwamba mkono wa Allah unafanana na mkono wa kiumbe katika hali yoyote ile, isipokuwa ni ufanano wa majina tu. Allah anasema: (Hakuna kinachofanana na yeye, na yeye ni mwenye kusikia sana mwenye kuona mno.[19]

## ADABU ZA KUZICHUNGA KWA ALLAH:

Muislamu huangalia zile neema za mwenyezi mungu kwae zsizo na idadi, amezipata kuanzia pale tu alipo wekwa katika mfuko wa uzazi wa mama yake akiwa tone la manii, na zinaendelea, akiwa nazo neema hizo hadi atakapokutana na Mola wake Mlezi, hivyo

[18] Hadithi imenukuliwa na Imamu Bukhary na Imamu Muslim
[19] Sura Shura (42) Aya ya 11

anamshukuru Allah Mtukufu kwa neema hizo kwa ulimi wake, kwa kushukuru na kumsifu, na kwa viungo vyake kuvifanya vimtumikie na kumtii Allah, basi hii inakuwa ni adabu mbele ya Allah Mtukufu, kwani si adabu kabisa kupinga neema za Allah, na kukaidi fadhila za mwenye kuneemesha. Allah anasema: (Basi nitajeni nitawataja na mnishukuru na msinikufuru)[20]

Na mwanadamu ana angalia elimu ya Allah Mtukufu kwake, na uwezo wake wakujua hali zake zote basi inapelekea moyo wake kujaa kumuogopa, na nafsi yake kupata utulivu na kumtukuza, basi ataogopa kumuasi na anaona aibu kutoka katika kumtii, basi huko ndio kuwa na adabu na Allah Mtukufu, kwani hakuna hata chembe ya adabu kwa mja kumdhihirishia maasi Bwana wake, au kumkabili na machafu na mabaya ili hali yeye anamuona. Allah anasema:

(Anayajua yaliyo mbinguni na ardhini. anayajua yale mnayo yaficha na mnayo yadhihirisha na Allah ni Mjuzi mno kwa yaliyomo vifuani)[21]

---

[20] Sura Al baqara (2) Aya ya 152

[21] Sura Attaghabuni (64) Aya ya 4

Na Muislamu anayaangalia yale makadirio aliyokadiriwa na Allah kuwa yatamtokea tu, na wala hana uwezo wa kuyakimbia, na wala hana wa kuegemea kwake wala wa kumuokoa ila Allah tu , basi anakimbilia kwake Mtukufu, na kuliacha jambo lake kwake na kumtegemea yeye tu, hii inakuwa ni katika kuchunga adabu na muumba wake. Kwani hakuna hata chembe ya adabu kumkimbia asiyekimbilika na kumtegemea asiye na uwezo wa aina yoyote wala kujiegemeza kwa asiye na uwezo na nguvu yoyote Allah anasema: (hapana kiumbe yeyote ila yeye anamwendesha atakavyo). Huud.
(Na kwa Allah tegemeeni ikiwa nyinyi ni Waumini (wa kweli)[22]

Na pia Muumini anaziangalia rehema za Allah kwake na kwa viumbe wote, basi anatumai kupata ziada kutokana na rehema hizo, basi ananyenyekea kwa unyenyekevu wa kweli na, kujikaribisha kwake kwa kauli nzuri na amali njema, basi hiyo inakuwa ni adabu na Allah, kwani si katika adabu hata kudogo kukata

[22] Sura Al maida (5) Aya ya 23

tamaa kuipata rehema za Allah zilizo nyingi na pana.

Na Muislam ana angalia ukubwa na ukali wa nguvu za Mola wake Mlezi na nguvu za kuangamiza kwake, basi anamuogopa kwa kufanya utiifu na kuto muasi, na hii inakuwa kwake ni adabu na Allah. Kwani si adabu hata kidogo kwa mja aliye dhaifu, asiyeweza chochote kujiingiza katika kumuasi na kumdhulumu Mola wake Mlezi aliye na nguvu Mwenye uweza wa kila kitu, na yeye anasema:
(...Na pindi Allah akitaka kuwapa watu (fulani) mtihani, hatapata sehemu ya kukimbilia, na wao hawana kinyume cha yeye msimamizi (mwingine atakaye wasimamia)[23]
Na anasema: (Hakika adhabu ya Mola wako Mlezi ni kali mno)[24]
Muislamu pia anamuona Allah pale anapo muasi na kutoka katika utiifu wake, kama vile makemeo yake yameshampata, na adhabu yake imeshamfika, kama vile anavyo muona wakati wa kutii na kufuata sheria zake kama

[23] Sura Arradi (13) Aya ya 11
[24] Sura Alburuji (85) Aya ya 12

kwamba ahadi zake kwake zimethibiti, na kana kwamba joho la radhi zake amelivulia, basi Muislamu huyu anakuwa Muislamu mwenye dhana nzuri kwa Allah, kwa vile si katika adabu hata kidogo mtu kuwa na dhana mbaya kwa Allah na akamuasi na kutoka katika twaa yake na anadhani kuwa hamfuatilii au yeye hachukuliwi hatua kutokana na madhambi yake naye anasema Allah: (...Na lakini mlidhani kuwa, hakika Allah hajui mengi kati ya mnayoyatenda. Na hilo kwenu ndio dhana yenu mbaya ambayo mliyo mdhania Mola wenu Mlezi, imekuangamizeni, basi mkawa miongoni mwa walio pata khasara.[25]

Kama ilivyo ni kwamba si katika adabu pamoja na Allah kumuogopa na kumtii, kisha adhani kuwa yeye hatamlipa kwa matendo yake mema, au yeye hata kubali twaa yake na ibada yake, na Allah Mtukufu ndie mwenye kusema:
(Na yeyote atakaye mtii Allah na Mtume wake, na akamuogopa Allah na akamcha, basi hao ndio walio faulu[26].

---

[25] Sura fusswulati (41) Aya ya 22-23
[26] Sura Annour (24) Aya ya 52.

Kwa ufupi ni kwamba: shukrani za Muislamu kwa mola wake mlezi kwa neema alizo mneemesha, na kumuonea haya mola wake pale anapovutika kufanya maasi, na kurejea kwake kwa ukweli kabisa, na kumtegemea na kutaraji rehema zake, na kuogopa adhabu yake, na kuwa na dhana nzuri kwa Allah juu ya utekelezaji wa ahadi zake kwake, na pia makemeo yake kwa anaye mtaka miongini mwa waja wake, Hivyo ndio kuchunga adabu kwa Allah, na kwa kadri ya kushikamana kwake na kuilinda ndio daraja yake na nafasi yake inapanda.

# KUWA NA ADABU KATIKA MANENO YA ALLAH

Muislamu ana amini utukufu wa maneno ya Allah Mtukufu, na ubora wake ulio juu ya maneno mengine yote, na kwamba Qur-ani ni maneno ya Allah, atakaye yasema atakuwa ameyasema ya kweli, na atakaye hukumu kwa maneno hayo atakuwa kafanya uadilifu, na watu wa Qur-ani ndio watu maalum wa Allah, na watakao shikamana nayo ndio walio faulu na wame okoka, na wanao yapuuza, wame hiliki na kupata khasara. Mtume - Allah amshushie rehema na amani- anasema: (Someni Qur-ani hakika hiyo qur-ani itakuwa muombezi kwa watu wake Siku ya Kiama[27]

Na kauli yake - Allah amshushie rehema na amani-: (Watu wa Qur-ani ni watu wa Allah na ni watu maalumu kwake.)[28]

Na kauli yake pia, - Allah amshushie rehema na amani-: (Hakika bila shaka kabisa nyoyo

[27] Hadithi imenukuliwa na imamu Muslim

[28] Hadithi imenukuliwa na imamu Ibnu Maajah

zinapata kutu, pakasemwa: Ewe Mjumbe wa Allah, ni vipi zitaondoka kutu hizo? Akasema: kwa Kusoma Qur-ani na kukumbuka kifo).

Na kwa sababu hii, basi hakika Muislamu na Qur-ani, zaidi ya kuwa Qur-ani ina halalisha mambo ya halali kwake, na ina haramisha yaliyo ya haramu, na anajilazimu kufuata adabu za Qur-ani na kujipamba na tabia za Qur-ani, kwa hakika yeye anajilazimu wakati wa kuisoma kufuata adabu zifuatazo**:**
**-** Na afanye pupa kadri awezavyo aisome akiwa na twahara (udhu), hali ya kuelekea qibla, na kukaa kwa adabu na utulivu**.**

- Aisome taratibu, asiwe na haraka wakati wa kuisoma kwake, hivyo asiisome (Qur-an yote) katika muda mchache sana chini ya siku tatu. Kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani**-:** (Hakufahamu yeyote aliye isoma qur-an (aliyehitimisha) chini ya siku tatu).[29]

---

[29] Hadithi imenukuliwa na imamu tirmidhy na Ibnu Maajah 2949,1347.

- Ajilazimu unyenyekevu na kuzingatia wakati wa kuisoma.

- Aisome kwa sauti nzuri, kwa kauli yake Mtume - Allah amshushie rehema na Amani-: (Ipambeni qur-ani kwa sauti zenu)

- Asidhihirishe kisomo chake endapo atahofia Riyaa (kujiona) au kuwakera wanao swali.

- Aisome kwa mazingatio, na kuwa dhahiri moyo wake, na kufahamu maana zake na siri zake.

- Ajitahidi asifike kwa sifa za watu wa Qur-ani, ambao ni watu maalum wa Allah.

# KUCHUNGA ADABU PAMOJA NA MTUME - WA ALLAH صلى الله عليه وآله وسلم

Mislamu anahisi utulivu wa nafsi yake, kwa kuwa na adabu kamili pamoja na Mtume wa Allah, Allah amshushie rehema na amani- nayo ni kwa sababu zifuatazo:

- Hakika Allah amemuwajibishia Muumini mwanaume na Muumini mwanamke kuwa na adabu na mtume- Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-, katika kauli yake Allah Mtukufu: (Enyi ambao mlio amini msitangulie mbele ya Allah na Mtume wake[30]

Na kauli yake: (Enyi ambao mlio amini, msinyanyuwe sauti zenu juu ya sauti ya Mtume, na msinyanyuwe sauti (wakati wa kuzungumza naye) kama mnapozungumza nyinyi kwa nyinyi, isije yakabatilishwa matendo yenu ilhali wenyewe hamjui.[31]

[30] Sura Al hujrati (49) Aya ya 1
[31] Sura Al hujrati (49) Aya ya 2.

Kwa hakika Allah amewawajibisha Waumini kumtii, na amewajibisha kumpenda, Allah anasema: (Enyi ambao mlio amini, mtiini Allah na mtiini Mtume ...) [32]

Na amesema: (na kile alichowaletea Mtume, basi kichukueni na alichowakataza, acheni...)[33]
Na kauli yake: (Sema ikiwa mnampenda Allah, basi nifuateni, Allah atawapenda na na atawasamehe madhambi yenu, na Allah msamehevu mno mwenye kurehemu sana)[34]

Na kwa hakika amesema Mtume - Allah amshushie rehema na amani-
(Hataamini mmoja wenu hadi niwe kipenzi zaidi kwake, kuliko mtoto wake na baba yake na watu wote.)[35]
Lakini vipi inakuwa adabu njema kwa Mtume Allah- amshushie rehema na amani-? Na inakuwa katika yapi?
- Itakuwa kwa utiifu kwake katika mapito yote ya dunia na akhera.

---

[32] Sura Annisaa (4) Aya ya 59.
[33] Sura Al hashri (59) Aya ya 7
[34] Sura Aali imran (3) Aya ya 31.
[35] Hadithi imenukuliwa na imamu Bukhary na Muslim

- Asitangulize mapenzi ya yeyote wala wala heshima na taadhima juu ya mapenzi na heshima na taadhima ya mtume – Rehema za Allah na Amani zimfikie-

- Kuwapenda wale ambao aliwapenda, na kuwachukia wale ambao aliwachukia, na Kumridhia Yule aliyekuwa anamridhia na kukasirishwa na kile kilicho kuwa kikimkasirisha.

- Kumtukuza kumheshimu wakati anapotajwa, na kumtakia rehema na amani.

- Kuya amini yote aliyo yaeleza miongoni mwa mambo ya dini na ya dunia, na mambo yaliyo jificha katika maisha ya dunia na akhera.

- Kuifufua sunna yake, kudhihirisha sheria zake, kufikisha daawa yake na kutekeleza wosia wake.

# ADABU KWA MASWAHABA NA WAUMINI:

Muislamu ana amini uwajibu wa kuwapenda Maswahaba wa Mtume -Allah amshushie rehema na amani-, na watu wa nyumbani kwake, na kuwa wao ni bora kuliko wengine katika Waumini na Waislamu, na kwamba pia wao wanatofautiana ubora na daraja kulingana na kutangulia kwao kuingia katika Uislamu.
Wabora wao zaidi ni Makhalifa (viongozi) wanne, kisha Maswahaba kumi waliyobashiriwa pepo nao ni Makhalifa viongozi wanne na Twalaa bin Abdullah, Zubeir bin Awwami, Saadi bin abi Waqqasi, Saidi bin Zaidi,Abuu ubaida bin Al jarrah, na Abdulrahmani bin Aufi, kisha wanao wafuatia ni wale walioshiriki vita vya Badri, kisha wale walio bashiriwa pepo kinyume na wale kumi, kama vile Fatma Azzahraa na watoto wake Al hassani na Hussein, Thabiti bin Qaisi na Bilali bin Rabaah na wengine.

Kama ambavyo Muislamu ana amini uwajibu wa kuwatukuza na kuwaheshimu Maimamu wa Kiislamu, na hao ndio viongozi wa dini, kama

vile wanazuoni wa fani ya Fiqih, wa Hadithi,na wa Tafsiri, miongoni mwa Tabiyna (kizazi kilichofuatia baada ya Maswahaba) na walio kuja baada yao -Allah awarehemu na awaridhie- wote.

Kama ambavyo Muislamu ana amini uwajibu wa kuwatii viongozi wa Mamlaka za Kislamu na kuwaheshimu,kushirikiana pamoja nao katika kupambania dini ya Allah bega kwa bega na kuto wahama na kuwa asi kwa kutoka katika utii wao.

Hivyo kila Muislamu anatakiwa kuwa na adabu maalum kwa hawa wote waliyotajwa: Maswahaba wa Mtume - Allah amshushie rehema na amani- na watu wa nyumbani kwake:

- Anawapende kwa sababu Allah na Mtume wake -Allah amshushie rehema na amani- wanawapenda watu hao.
- Ana amini ubora wao ulio juu ya wengine, miongoni mwa Waumini na Waislamu, kutokana na kauli yake Allah Mtukufu:" Na wale waliyotangulia ambao ni wa mwanzo miongoni mwa Wahamiaji na Answari (wakazi wa

Madina) na wale ambao wamewafuata hao kwa wema, Allah amewaridhia, na amewa andalia pepo"...[36]

Na kwa kauli yake Mtume Allah amshushie rehema na amani,

"Msiwatukane Maswahaba wangu, na kwa hakika kabisa lau mmoja wenu angetoa (sadaka) dhahabu mfano wa Mlima Uhudi, kisingewiana alichotoa na kibaba alichotoa mmoja wao, au nusu yake".[37]

- Anatakiwa amuone Abubakri ndie mbora wa Maswahaba wote, kisha Omar kisha Othmani kisha Ally, Anasema Ibnu Omar Allah amridhie (Tulikuwa enzi za Mtume -Allah amshushie rehema na amani- tunaona kuwa mbora wa umma huu baada ya Mtume wetu ni Abubakri kisha Omar kisha Othman kisha tunanyamaza".[38]
- Muislamu anatakiwa kuacha kabisa kuzungumzia mabaya yao, na anyamazie tofauti zilizotokea kati yao.

---

[36] Sura Attaubah (9) Aya ya 100

[37] Hadithi imenukuliwa na Abuu Daudi

[38] Imenukuliwa na imamu Al bukhary

- Muislamu anatakiwa kuamini heshima ya wake wa Mtume -Allah amshushie rehema na amani-, kwamba wao ni wasafi, wema na aone kuwa aliye bora zaidi kati ya wake wa Mtume ni mama Khadija binti Khuwailadi, na Aisha binti Abubakri.

**AMA KWA UPANDE WA MAIMAMU WA KIISLAMU MIONGONI MWA WASOMAJI QUR,ANI,WATU WA FANI YA HADITHI, WATU WA FIQIH NA WENGINEO, KWA HAKIKA NI KUWA:**

- Muislamu anawapenda, na kuwatakia rehema, na kukubali kuwa ni watu wenye ubora.
- Asiwataje isipokuwa kwa jambo la kheri, na asitie dosari katika kauli au rai zao, na anatakiwa ajue kuwa wao walikuwa wanajitahidi na walikuwa na IKHLASI, na aitangulize rai yao juu ya rai ya wengine, waliyokuja baada yao, na asikatae kauli zao isipokuwa tu kama zimepingana na kauli ya Allah au kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-, au kauli za Maswahaba wake -Radhi za Allah ziwe juu yao- wote.

- Ama walio kuwa chini yao, ni maimamu wanne: Maliki, Ashaafy, Ahmad na Abuu Hanifa, na walicho kisema katika masuala mbali mbali ya dini, fiqih na sheria, yame toholewa kutoka katika kitabu (qur-ani) na sunna (Hadithi) za Mtume wake - Allah amshushie rehema na amani-, na wao hawana la kwao isipokuwa tu yale waliyo yafahamu kutoka misingi miwili (Qur-an na Hadithi) au waliyo yanyambua kutoka humo au kwa kulinganisha na yaliyomo humo.
- Muislamu anatakiwa aone kuwa wao ni wanadamu, hivyo wanapatia na kukosea, mmoja wao anaweza kukosea haki katika moja ya maswala, si kwa kukusudia na makusudi- waepushwe na hilo- lakini anaweza kukosea kwa kusahau au kutolijua jambo sawa sawa, na kwa sababu hii Muislamu hatakiwi kuwa kinganganizi wa rai ya mmoja wao na kuacha ya wengine, bali inampasa kuchukua rai ya yeyote kati yao.

## AMA VIONGOZI WENYE MAMLAKA:

- Muislamu anatakiwa kuona uwajibu wa kuwatii, kwa kauli ya Allah: " Enyi ambao mlioamini, mtiini Allah na mtiini Mtume, na viongozi wenye mamlaka miongoni mwenu, na endapo mtatofautiana katika jambo, basi lirudisheni (hukumu yake) kwa Allah na Mtume, ikiwa nyinyi (kweli) mnamuamini Allah na Siku ya Mwisho, (kufanya hivyo) ni kheri kwenu na utatuzi uliyo bora (wa tofauti zenu)" . Na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-,

"Sikieni na mtii, hata kama mtatawaliwa na mtumwa wa kihabeshi (nywele) za kichwa chake kama kwamba zabibu".[39]
Lakini Muislamu hatakiwi kuona inafaa kuwatii kwenye maasi ya Allah Mtukufu, sababu kumtii wa Allah kunatangulizwa juu ya kuwatii wao, amesema Mtume - Allah amshushie rehema na amani,: "Hakuna kumtii kiumbe ikiwa kumtii huko kuna kumuasi Yule aliyeumba".[40]

---

[39] Hadithi imenukuliwa na imamu Bukhary
[40] Hadithi hii imenukuliwa na imamu Abuu Daudi Atwayalis na katika Musnadi ipo namba 856

- Anatakiwa kuona uharamu wa kuasi watawala, au kutangaza uasi dhidi yao, kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-: "Yeyote atakayechukia kwa mtawala wake chochote, basi asubiri, kwa sababu yeyote atakaye muasi mtawala, atakufa kifo cha kijahili[41]"

- Anatakiwa kuwaombea dua wawe wema, na kupatia katika kuongoza kwao, na waepushwe na na shari, sababu kustawi kwa umma kunategemea kustawi kwa watawala, na kuharibika umma ni kwa kuharibika wao.

- Anatakiwa kuipambania dini ya Allah pamoja nao, na aswali nyuma yao, hata kama watakuwa waovu na wanafanya mambo ya haramu, ambayo hayamtoi kwenye Uislamu, kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-, alipo ulizwa kuhusu kumtii mtawala: "..sikilizeni na mtii, kwa hakika wao wana mizigo yao waliyo ibeba, nanyi mna mizigo yenu mliyo ibeba. [42]"

---

[41] Hadithi imenukuliwa na imamu Bukhary na Muslim
[42] Imenukuliwa na imamu Muslim 12

Na kwa kauli ya Ubada bin Al-Swamiti: "Tumempa kiapo cha utii Mtume kwamba: Tutamsikiliza na kumtii katika hali ya furaha na kuchukizwa , katika ya umaskini na utajiri, na pia tusimuasi mtawala na kutoka katika utii wake.[43]

Akasema:Isipokuwa kama mtakapo ona ukafiri wa wazi, mna nyinyi ushahidi wa hilo kutoka kwa Allah [44]"

---

[43] Imenukuliwa na imamu Bukhary 1511
[44] Imenukuliwa na Bukhary 1482-Muslimu 42.

# MUISLAMU NA NAFSI YAKE:

Muislamu ana amini kwamba maisha yake bora ya duniani na akhera msingi wake ni kuipa adabu mzuri na kuisafisha nafsi yake, Allah amesema: "Hakika amefaulu Yule aliyeitakasa (nafsi yake kwa matendo mema) na ametoka tupu Yule aliyeipoteza (kwa maasi).[45]
Na amesema:
"Allah anaapa kwa wakati wa swala ya alaasri, kwa hakika mwanadamu yupo katika khasara, isipokuwa tu wale walioamini na wakatenda amali njema, na waka usiana haki na waka usiana kufanya subira.[46]

Na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:
"Watu wote katika umma wangu wataingia peponi isipokuwa tu Yule atakayekataa, pakasemwa: ni yupi atakaye kataa ewe Mjumbe wa Allah? Akasema: atakayenitii ataingia peponi na atakayeniasi, kwa hakika kabisa huyo amekataa."

---

[45] Sura ashamsi (91) Aya ya 01-10.
[46] Sura Al asri (103) Aya ya 1-3

Kama ambavyo Muumini anatakiwa kuamini kuwa kunacho isafisha nafsi yake na kuitakasa, ni imani tu, na hakika kinacho ichafua na kuiharibu ni ukafiri na maasi. Allah amesema: "Dumisha swala (wakati wa) ncha mbili za mchana na nyakati za usiku, hakika ya mema yana ondoa maovu huo ni ukumbusho kwa wenye kukumbuka[47]
"Bali maasi yamezunguka nyoyo zao(hadi zinakufa) kwa sababu ya yale waliokuwa wakiyachuma. [48]

Na kwa sababu hii basi Muislamu anatakiwa siku zote, kuipa adabu mzuri nafsi yake na kuilazimisha kufanya kheri na kujiweka mbali na shari, usiku na mchana, na kuitathmini kila wakati, na aiingize katika matendo ya kheri, na aipe msukumo hasa katika kutenda utiifu, kama ambavyo anatakiwa kuiweka mbali sana na shari na mambo yanayo iharibu. na katika hilo afuate hatua zifuatazo:

1- Kuleta toba: nako ni kwa kujiweka mbali na madhabi na maasi yote, kujutie kila dhambi

[47] Sura Hudi (11) Aya ya 114.
[48] Sura Almutwafifina (83) Aya ya 14

iliyopita, na kuazimia kutorudia tena dhambi hizo siku zijazo Allah anasema:
(Enye ambao mlio amini, rudini kwa Allah kwa toba ya kweli, hakika (mkifanya hivyo) Mola wenu Mlezi atakufutieni madhambi yenu, na atawaingiza katika pepo ipitayo chini yake mito..[49]

Na kutokana na kauli yake Mtume -Allah amshushie rehema na amani:
(Hakika Allah ananyoosha mkono wake usiku ili atubu Yule aliyefanya makosa mchana, na ananyoosha mkono wake mchana, ili atubu Yule aliyekosea usiku, hadi jua lichomoze upande wa maghribi".[50]”

2- Kujichunga: nako ni Muislamu kujichunga na mola wake mlezi wakati wote katika maisha yake, na ajue ya kwamba Allah anamuona, anajua siri zake na mambo yake ya dhahiri, na kwa hali hiyo nafsi inakuwa na yakini kuwa inachungwa na Allah mtukufu, itahisi raha kumtaja, na itapata raha katika kumtii, na

[49] Sura Attahrimi (66) Aya ya 8
[50] Hadithi imenukuliwa na imamu Muslimu.

kupuuzia vyoote visivyo kuwa Allah, na hii ndio maana ya kujisalimisha kwa Allah, pale aliposema: "Na ni nani aliye na dini mzuri zaidi kuliko Yule ambaye ame usalimisha uso wake kwa Allah ilhali yeye ni mwema..[51]

Nayo ndio aliyoisema Allah Mtukufu:"Na huwi (Ewe Muhammad) katika jambo lolote, na wala husomi chochote miongoni mwa Aya za qur-ani, na wala hamtafanya amali yoyote (ya kheri au shari) isipokuwa tu sisi ni mashahidi pale mnapo shughulika nayo.[52]
Na kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na Amani-: (Umuabudu Allah kama unamuona, na kama humuoni basi yeye anakuona.[53]

3- Kujitathmini: nako ni kwamba zama alipokuwa Muislamu anafanya amali mbali mbali katika haya maisha, usiku na mchana, ili apate kile kitakacho mfanya aishi vizuri katika nyumba ya akhera, na kumuwezesha kupata karama na

---

[51] Sura Annisaa (4) Aya ya 125
[52] Sura Yunus (10) Aya ya 10
[53] Hadithi imenukuliwa na imamu Bukhary na Muslimu

radhi za Allah humo, na ilipokuwa dunia ndio msimu wake wa kutenda amali, basi ni wajibu wake aangalie yaliyo ya wajibu kwake, kama vile tajiri anavyoangalia msingi wa mali yake, na aangalie mambo ya sunna kama ambavyo tajiri anavyo angalia faida zinazozidi kuingia katika msingi wake. Na aangalie maasi kama inavyo angaliwa hasara kwenye biashara, kisha akae peke yake faragha mara kwa mara, aifanyie tathmini nafsi yake katika matendo ya siku yake,  endapo ataona mapungufu ailaumu na kuikemea, na asimame kidete kuziba hayo mapungufu mara moja, likiwa ni jambo linaloweza kulipwa alilipe, na endapo si jambo linaloweza kulipwa basi ailazimishe nafsi yake kukithirisha sunna mbali mbali, na kama ataona mapungufu yake yapo katika sunna basi arekebishe hayo mapungufu, na kama ataona mapungufu yake yapo katika  kujiingiza katika yale yaliyokatazwa, basi atake msamaha na ajutie, na arudi na afanye mambo ya kheri yatakayo ziba na ku tengeneza pale alipoharibu, hii ndio maana ya kufanya tathmini katika nafsi. Na miongoni mwa dalili ni kauli ya Allah Mtumukufu: (Enyi ambao mliyoamini

mcheni Allah, na nafsi itazeme kile ambacho imekitanguliza kwa ajili ya kesho (akhera), na mcheni Allah, hakika Allah ni mwenye habari mno kwa yote mnayo yatenda.[54]
Na Omar – Allah amridhie- amesema: (Zitathmini nafsi zenu, kabla hazijatathminiwa"

4- Kupambana: nako ni binadamu kuifanya nafsi yake ndio adui yake mkubwa, na kwa hakika nafsi ilivyo kiuhalisia ni yenye kumili sana kwenye shari hali ya kuikimbia kheri, ina amuru sana maovu na kupenda raha, na kuegemea katika matamanio ya nafsi, hata ikiwa humo ndio kuna ubaya wake. Basi Muislamu akilijua hilo apambane na nafsi yake katika kufanya ya kheri, na kujiweka mbali na maovu Allah anasema:

(Na wale waliopambana kwa ajili yetu, hakika bila shaka tutawaongoza katika njia zetu, na hakika Allah yupo pamoja na watendao mema).[55]

---

[54] Sura Al mujaadila (59) Aya ya 18
[55] Sura Al ankabuti (29) Aya ya 69

Haya ndio mapito ya waja wema na njia ya waumini wa kweli, Mtume –
Allah amshushie rehema na amani-, anasimama usiku ana swali hadi miguu yake mitukufu inavimba, na alipoulizwa katika hilo, alijibu "Kwa nini nisipende kuwa mja mwenye shukurani mno."

## HAKI ZA WAZAZI WAWILI:

Muisilamu anazikubali na kuziamini haki za wazazi wawili na wajibu wake kwao, kuwafanyia wema na hisani na kuwatii, si kwa sababu wazazi ndio sababu ya yeye kuwepo duniani au kwa sababu wamemfanyia mazuri yanayo wajibisha kwake kuwalipa mfano wa hayo, bali ni kwa sababu Allah amewajibisha kuwatii, amesema Allah Mtukufu:
(Amehukumu Mola wako Mlezi kwamba msiabudu chochote isipokuwa yeye tu, na wazazi wawili muatendee wema..[56]
Na Mtume - Allah amshushie rehema na amani- amesema: (Je! Nikuambieni dhambi kubwa zaidi kati ya madhambi?, wakasema ndio Ewe

[56] Sura Al isaraa (17) Aya ya 23.

mjumbe wa Allah, akasema: kumshirikisha Allah na kutowatendea wema wazazi wawili”.[57]

Na amesema Abdullah bin Masouud Allah amridhie kwamba, ”nimemuuliza Mtume - Allah amshushie rehema na amani-, ni amali ipi inapendeza zaidi kwa Allah Mtukufu?,“ akasema kuwafanyia wema wazazi” nikasema kisha nini? akasema jihadi kupigania dini ya Allah’.

Na alikuja mtu kwa Mtume - Allah amshushie rehema na amani-, akimtaka idhini aende kwenye jihadi akamwambia: “je wazazi wako wapo hai? akajibu ndio, akasema: wapambanie hao (wazazi)” [58].

Na Muislamu anapotambua haki hii kwa wazazi wake, na akaitekeleza kikamilifu, kwa kumtii Allah na kwa ajili ya kutekeleza wasia wake, kwa hakika analazimu pia upande wa wazazi wake adabu zifuatazo:

- Kuwatii wao kwa kila amri anayo amrishwa nao, au wanayo mkataza, ikiwa tu sio kumuasi

---

[57] Imenukuliwa na imamu Bukhary na Muslim
[58] Imenukuliwa na imamu Bukhary na Muslim

Allah Mtukufu, na sio kwenda kinyume na sheria yake, kwani hakuna kumtii kiumbe katika jambo linalo muasi Muumba. Na kwa kauli yake Allah: (Na kama watakulazimisha kunishirikisha kwa jambo ambalo huna elimu nalo, basi usiwatii (katika jambo hilo) na suhubiana nao hapa duniani kwa wema). [59]
Na kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-: (Hakuna kumtii kiumbe katika jambo linalo muasi Muumba).

- Kuwasikiliza na kuwa na adabu nao, kuwa laini na kuwafanyia upole, kuwa kirimu kwa vitendo na kauli, asinyanyue sauti yake kuwa juu ya sauti yao, asitembee mbele yao, asiruhusu kukerwa na mke au mtoto, kuwaomba ruhusa na kuwataka ushauri, na kufuata rai zao.

- Kuwafanyia kila aina ya wema na hisani kwa kadri awezavyo, kama kuwapa chakula na kuwavisha na kuwatibu magonjwa yao kuwaondolea kero walizo nazo na kujitoa kwa ajili yao.

- Kuwaombea dua na kuwatakia msamaha kwa Allah,na kuwa kirimu marafiki zao.

[59] Sura Luquman (31) Aya ya 15.

# HAKI ZA WATOTO:

Muislamu anatambua kwamba mtoto, awe wa kiume au wa kike, ana haki na wajibu kwa baba yake, na zina anzia katika kumchagua mama wa mtoto huyo, na kumpa jina zuri pindi anapozaliwa, na kumfanyia ibada ya kichinjwa cha AQIQA, na ni bora zaidi ikawa siku ya saba baada ya kuzaliwa kwake, Na kumhitani mtoto wa kiume, na kumfanyia huruma na upole, na kumpa matumizi, na kumlea vizuri, na kutilia umuhimu ajue utamaduni na elimu ya kiislamu, kumzoesha kutekeleza mambo yake ya wajibu na ya sunna, na kuhimiza kumwozesha atakapofikia umri wa kuoa au kuolewa, na dalili katika hayo yaliyotajwa ni nyingi miongoni mwa hizo ni kauli ya Allah: (Na kina mama wa watoto (wanao nyonya) wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili, kwa anayetaka kukamilisha kunyonyesha. Na ni wajibu wa baba wa mtoto kuwalisha na kuwavisha kwa maarufu) .[60]

---

[60] Sura Albaqra (2) Aya ya 233.

Na kauli yake: (Enyi ambao mlio amini zilindeni nafsi zenu na watoto wenu na moto, ambao kuni zake ni watu na mawe).[61]
Na kauli yake: (Na msiwauwe watoto wenu kwa kuhofia ufukara, sisi tuna waruzuku wao na ninyi)..[62]

Na kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-: (Mtoto atakuwa rehani kwa Aqiqa yake, ambayo atachinjiwa siku ya saba, na atapewa jina na kunyolewa nywele zake siku hiyo).[63]

Na kauli yake: (Fanyeni usawa kati ya watoto wenu katika vile mnavyo wapa ). [64]

Na akasema Mtume: (Waamrisheni watoto wenu kuswali wakiwa na umri wa miaka saba, na wapigeni (endapo hawataswali) wakiwa na miaka kumi, na watenganisheni katika vitanda wakati wa kulala).[65]

---

[61] Sura Attahrimu (66) Aya ya 6.
[62] Sura Alsraa (17) Aya ya 31
[63] Imenukuliwa na watu wa sunani.
[64] Imenukuliwa na Albahaqy na Tabarany
[65] Imenukuliwa na Abudaudi.

## HAKI ZA NDUGU:

Muislamu anatakiwa kuona kuwa heshima kwa ndugu ni sawa na heshima kwa baba na watoto, hivyo ndugu mdogo ana haki ya kuheshimiwa sawa na ndugu mwenye umri mkubwa, kama wanavyo heshimiwa baba zao, na ndugu wakubwa wanapasa kuwapa heshima ndugu zao wadogo, kama heshima aliyokuwa nayo baba, miongoni mwa haki na wajibu na adabu. hilo ni kutokana na mapokezi kutoka kwa Mtume: (Mfanyie wema mama yako na baba yako, kisha dada yako na kaka yako kisha walio chini yako) .[66]

## HAKI ZA WANA NDOA:

Muislamu akubali adabu wana zobadilishana wana ndoa (mke na mume), nazo ni haki za kila mmoja wao kwa mwenzake, hilo ni kwa kauli ya Allah Mtukufu: (Na wana wao haki (za kutekelezewa) mfano wa wajibu waliokuwa nao, kwa wema...[67]

---

[66] Imenukuliwa na Al hakim katika kitabu (Kanzu alummal 16/474 na 580

[67] Sura Al baqara (2) Aya ya 228

Aya hii imethibitisha kuwa, kila mmoja kati ya wana ndoa wawili ana haki kwa mwenzake, na mwanaume amezidishiwa daraja moja, kwa mazingatio maalumu.
Na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani katika Hija ya kuaga: (Eleweni kwamba mna nyinyi haki kwa wake zenu, na wake zenu wana haki kwenu) .[68]
Isipokuwa baadhi ya hizi haki wana shirikiana wana ndoa wote wawili na zingine hawa shirikiani ni mahsusu kwa kila mmoja wao.
Basi haki wanazoshirikiana ni:

1- Uaminifu: ni wajibu kwa kila mwana ndoa awe muaminifu kwa mwenza wake asimfanyie hiana yoyote, kwenye dogo au kubwa.

2- Mapenzi na huruma: kiasi kila mmoja abebe mapenzi na huruma kikamilifu kwa mwenza wake, na watabadilishana hayo kati yao muda wote wa maisha yao. Hayo yapo katika kauli ya Allah Mtukufu: (Na miongoni mwa ishara za uwezo wake, amewaumbieni kutokana na

[68] Hadithi imenukuliwa na Attirmidhiy

nyinyi wenyewe wake, ili iwe kitulizo kwenu na amejaalia kati yenu mapenzi na huruma)..[69]
Na uthibitisho wa kauli ya Mtume anaposema: (Asiyekuwa na huruma naye hahurumiwi) [70]

3- Kuaminiana: kila mmoja amuamini mwenza wake, haingiwi na shaka yoyote katika ukweli wake, nasaha zake na undani wake, hiyo ni kufuatia kauli ya Allah Mtukufu: (Hakika ya Waumini ni ndugu...) [71]

Na kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-: (Hatokuwa mkamilifu wa imani mmoja wenu, mpaka ampendelee mwenzake kile anacho kipendelea katika nafsi yake ''.[72]

Na mahusiano ya ndoa yanayazidi mahusiano ya imani, kiuaminifu na nguvu na uzito.
Adabu zingine kwa ujumla ni uwa mpole katika kuamiliana, bashasha usoni, ukarimu na

---

[69] Sura alroum (30) Aya ya 21
[70] Hadithi imenukuliwa na attabrany
[71] Sura Al hujrati (49) Aya ya 10
[72] Hadithi imenukuliwa na imamu Bukhary, Muslimu na wengine.

heshima. Na hizo ndizo adabu ya kuishi pamoja kwa wema ambazo Allah ameziamrisha katika kauli yake:( Na ishini nao kwa wema…) [73]
Nako ni kuusiana kheri ambayo ameiamrisha Mtume Mtukufu katika kauli yake: (Wauseini wanawake kheri.) [74]
Na ama haki maalum na adabu ambazo zinazo mlazimu kila mmoja katika wanandoa, kuzisimamia, kwa mwenzake nazo ni:

## HAKI ZA MKE:

1- Kuishi naye kwa wema: kwa kauli yake Allah Mtukufu: (...Na ishini nao kwa wema...), basi inampasa ampatie chakula na mavazi anapo hitajia, na apupie kumuelimisha na kumfunza adabu.
Hilo ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume wa Allah, - Allah amshushie rehema na amani-, kwa Yule aliye muuliza: Ni ipi haki ya mke, anayo paswa mume amtekelezee?
Akamjibu: (Kumlisha anapohitaji chakula, na kumvisha anapohitaji kivazi na usimpige usoni,

[73] Sura Annisaa (4) Aya ya 19.
[74] Hadithi imenukuliwa na imamu Muslim

wala usimfanye kuwa ni mbaya, na usimuhame isipokuwa tu iwe (humo humo) ndani ya nyumba).[75]

Na kauli yake Mtume pia:( Eleweni, ya kwamba haki yao kwenu kuwafanyia vizuri kwenye mavazi na kwenye chakula) .
Na kauli yake: (Muumini mwanaume asimbughudhi Muumini mwanamke. Kama akichukia kwa mwanamke huyo tabia Fulani, basi mwingine itampendeza”.

2- Amfundishe mambo ya msingi ya dini yake kama atakuwa hayajui kabisa, au amruhusu kuhudhuria madarasani ili ajifunze, kwa vile mahitajio ya kujifunza dini yake, hayapungui uzito na umuhimu wa kupata kwake chakula na kinywaji. Allah anasema: (Enyi ambao mlio amini zilindeni nafsi zenu na watoto wenu na moto, ambao kuni zake ni watu na mawe.). [76]

3- Amlazimishe kutekeleza mafundisho ya Kiislamu, amzuie kutembea hali ya kuwa kavaa mavazi yasio ya staha, na kumzuia kukaa na

---

[75] Hadithi imenukuliwa na Abuudaudi
[76] Sura Attahrimu (66) Aya ya 6.

watu wasio maharimu zake, na mengineyo mfano wake…, Sababu mwanaume ni mchunga mwenye jukumu la kumhifadhi na kumlinda mwanamke. Allah anasema: (Wanaume ndio haswa wasimamizi wa wanawake ).[77]
Na kwa kauli yake Mtume -Allah amshushie rehema na amani-: (Mwanaume anajichunga mwenyewe na ataulizwa kuhusu anacho kichunga).

## HAKI ZA MUME:

Ni wajibu kwa mwanamke kwa mumewe kuchunga haki zifuatazo:

1- Kumtii katika mambo yasio kuwa ya kumuasi Allah. kwa kauli yake Allah: (Na endapo wata kutiini basi msiwatafutie njia ya kuwaudhi bila ya sababu…) [78]
Na kwa kauli ya Mtume wa Allah - Allah amshushie rehema na amani-:
"Pindi mwanaume atapomuita mkewe kitandani na akakataa, akawa hakwenda, akalala mwanaume

[77] Sura Annisaa (4) Aya ya 34.
[78] Sura Annisaa (4) Aya ya 34.

huyo akiwa amemkasirikia mkewe, basi Malaika watamlaani mwanamke huyo hadi kuche.
Na pia kwa kauli yake: (kama ningekuwa naweza kumuamuru yeyote kumsujudia mwingine, basi ninge muamuru mwanamke amsujudie mumewe”.[79]

2- Kulinda heshima na hadhi ya mume, na kuhifadhi na kuzilinda mali zake, watoto wake na mambo yote ya nyumbani kwake.
Kwa kauli yake Allah: (Basi wanawake wema, watiifu wenye kuhifadhi utiifu wao kwa waume zao hata wasipokuwepo, kwa kuwa Allah ameamrisha wazihifadhi). [80]

Na kwa kauli ya Mtume Allah amshushie rehema na amani, (Mwanamke ni mchunga katika nyumba ya mumewe, na ataulizwa kuhusu uchunga huo.” [81]

3- Kubaki katika nyumba ya mumewe, na kutotoka isipokuwa kwa idhini yake na ridhaa yake, na kuinamisha macho yake na kupunguza

[79] Hadithi zimenukuliwa na imamu Bukharin a Muslim
[80] Sura Annisaa (4) Aya ya 34.
[81] Hadithi imenukuliwa na imamu Bukhary

sauti yake, na kuamiliana na ndugu wa mumewe kwa wema, Allah anasema: (Na tulieni majumbani mwenu, na msijishaue kwa mishauwo ya kijahiliya).[82]
Na Kauli yake Allah Mtukufu: (...Na msizungumze na watu (wasiokuwa maharimu wenu) kwa sauti laini inayotia tamaa katika moyo wa yule ambae ana maradhi ya kupenda uovu..[83]
Na kauli yake:( Allah apendi kwa mtu yeyote kudhihirisha uovu wa maneno) ..[84]

Na kauli yake: (Na waambie wanawake Waumini wainamishe macho yao chini, na wahifadhi tupu zao na wasi oneshe mapambo yao isipokuwa yale yaliyo dhahiri tu…) [85]
Na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-: (Mwanamke bora ni Yule ukimtazama unafurahi, na unapo muamuru anakutii, na unapokuwa haupo anakuweka moyoni mwake, na kuhifadhi mali yako).[86]

---

[82] Sura Al ahzaab (33) Aya ya 33
[83] Sura Al ahzaab (33) Aya ya 32
[84] Sura Annisaa (4) Aya ya 148
[85] Sura Annour (24) Aya ya 31
[86] Hadithi imenukuliwa na imamu Atbrany

# ADABU PAMOJA NA NDUGU WA KARIBU:

Muislamu anashikamana na jamaa zake kwa adabu zile zile anazoshikamana nazo kwa wazazi wake, mwanawe na ndugu zake, hivyo ana amiliana vizuri na shangazi yake na mama yake mdogo kama anavyo amiliana vizuri na mama yake, na anamtendea wema ami yake na mjomba yake kama anavyomtendea wema na hisani baba yake.

Na kila anao ungana nao katika udugu muislam au sio muislam, anamzingatia kuwa ni miongoni mwa wenye kustahiki huruma, na kutengamana nao kwa wema.

Mgonjwa kati yao anamtembelea na kumliwaza na kumwombea ponyo, na aliye pata majanga na misiba mbali mbali humhani na kumpa pole, anamheshimu na kumsikiliza mkubwa kati yao,na kumhurumia aliye mdogo, ana waunga udugu hata kama wakimkata udugu, anakuwa mpole na laini kwao hata kama wakiwa wakali kwake, haya yote ni kwendana na mafunzo ya

Qur-ani tukufu na Hadithi za Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:
Anasema Allah: (Na muogopeni Allah ambaye kwaye mnaombana, na tahadharini na udugu)[87]

Na kwa kauli yake: (Na watu wakaribu wape haki zao )...[88]
Na kauli yake Allah: (Hakika Allah anaamuru uadilifu na ihsani na kutoa kuwapa ndugu wa karibu ...) [89]

Na kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:" (Sadaka unayo mpa masikini yeyote ni sadaka, lakini sadaka unayo mpa ndugu masikini, ni sadaka na ni kuunga udugu).

Na alisema pia kumwambia Asmaa biti Abuubakri - Allah amuiye radhi na baba yake- pale alipomuuliza kuhusu kumkirimu mama yake wakati alipofika Madinah akitokea Makkah, hali ya kuwa huyo mama yake ni mshirikina, alimwambia: (Ndio muunge udugu (mkirimu) mama yako),

---

[87] Sura Annisaa (4) Aya ya 1
[88] Sura Al israa (17) Aya ya 26
[89] Sura Annahli (16) Aya ya 90

# KUCHUNGA ADABU ZA JIRANI:

Muislamu anatakiwa kukubali haki wajibu za jirani kwake, na kumpatia kila mmoja haki hizo kikamilifu , hayo ni kwa mujibu wa kauli yake Allah mtukufu: (..na wazazi wawili kuwafanyia wema, na ndugu wa karibu na mayatima na masikini na jirani ndugu na jirani wa kuishi naye karibu..) [90]

Na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-: (hakuacha Jibrilu kuniusia kuhusu jirani hadi nikadhani kwamba atamrithisha). Anakusudia mali yake akifa.
Na miongoni mwa haki za jirani ni:

1- Ni kuto muudhi kwa kauli au kitendo, Mtume - Allah amshushie rehema na Amani- anasema: "Yeyote anaye muamini Allah na kuiamini Siku ya mwisho, basi amkirimu jirani yake).
Na kauli yake:

(Yeyote anayemuamini Allah na Siku ya mwisho, basi asimuudhi jirani yake)

---

[90] Sura Annisaa (4) Aya ya 36

Na akasema pia: "Naapa kwa Allah, si mkamilifu wa Imani, Naapa kwa Allah, si mkamilifu wa Imani. pakasemwa ni nani ewe Mjumbe wa Allah? Akasema ni Yule ambae jirani yake hana amani na shari yake).

2- Kumfanyia wema, hilo ni kwa kumnusuru anapo omba msaada, na amtembelee atapo umwa, ampongeze wakati wa furaha, amuhani anapo pata msiba na amsaidie anapo hitaji kusaidiwa, wanapokutana aanze kumsalimia, azungumze naye kwa upole, awe mpole anapozungumza na mtoto wake, na amuongoze katika yale yanayo tengeneza dini yake na dunia yake, na kusamehe mapungufu yake, na hatakiwi kufuatilia aibu zake, na asimbane katika ujenzi wa nyumba yake, au njia ya kupita, na asimuudhi kwa kutupa taka mbele ya nyumba yake, hayo yote ni katika ihsani kwake iliyoamrishwa.

3- Kumkirimu kwa kumpatia mema na kheri kwa kauli ya Mtume Allah amshushie rehema na amani: (Enyi wanawake wa Kiislamu asimdharau jirani wema wowte kwa jirani yake, hata kwa kumpa kitu kidogo kama ugoko wa mbuzi’

Na kauli yake alipomwambia Abi dharry: (Ewe Abadharry utakapo pika mchuzi, zidisha maji yake na mgawie jirani yako).
Na kauli ya Mtume kwa mama Aisha alipo muuliza: nina majirani wawili yupi nimpe haki zaidi akajibu:
(Mpe aliye karibu zaidi mlango wake na wako).

4- Umheshimu na kumpa hadhi, usimzuie kuweka ubao au mti kwenye ukuta wake, na asiuze au kupangisha chochote kinacho ungana naye isipokuwa tu baada ya kumfahamisha na kumshauri, kufuatia kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani: (Mmoja wenu asimzuie jeraji yake kuweka ubao wake katika ukuta wake).

Na kauli yake: (Yeyote atakaye kuwa jirani yake anapakana nae , au ni mshirika wake katika mali, hapaswi kuiuza isipokuwa baada ya kumuelezea jirani yake huyo.) [91]

---

[91] Hadithi imenukuliwa na imamu Al hakim na ameihasahihisha.

# ADABU ZA MUISLAMU NA HAKI ZAKE:

Muislamu anatakiwa kuamini na kuzichunga haki na wajibu kwa ndugu yake Muislam, hivyo amtekelezee haki hizo ndugu yake muislamu, huku aki amini kuwa kufanya hivyo ni ibada na Sadaka kwa ajili ya Allah mtukufu,
Na miongoni mwa haki hizo na adabu ni hizi zifuatazo:

1- Amsalimie pindi atakapokutana naye, kabla hajazungumzisha lolote, aseme "Assalamu alaykum warahmatullah wabarakaatuh," amani iwe juu yako na rehema za Allah na Baraka zake, huku akimpa mkono. Naye atajibu kwa kusema "waalaykumu salamu warahmatullah warakaatuh" na iwe kwako amani na rehema za Allah na Baraka zake. Hilo ni kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu:
(Na pindi mtakapo amkiwa, basi rudisheni maamkizi mazuri zaidi ya hayo au rudisheni kama hayo…).
Na kwa kauli ya Mtume - Allah ashushie rehema na amani:

(Aliye kwenye kipando amsalimie anayetembea na analiyetembea amsalimie aliyekaa, na wachache wawa salimie wengi)
Na kwa kauli yake pia mtume: (mtolee salamu unaye mjua na usiye mjua).[92]

2- amtakie dua anapotoa chafya, kama atamshukuru Allah kwa kusema: (Alhamdulillah) baada ya chafya, atamwambia (yarhamuka llahu) Allah akurehemu, na mtoa chavya atajibu: (yarhamukumu llahu wa yuswilihu baalakum) Allah akuongozeni awatengenezee hali zenu.

Kwa kauli yake Mtume Allah amshushie rehema na amani:
(Pindi anapopiga chafya mmoja wenu, basi ndugu yake aseme, yarhamuka llahu, (Allah akurehemu), na akisema kumwambia: Allah akurehemu basi amwambie: yahdiykumullahu wa yuswilihi baalukum (Allah akuongozeni awatengenezee hali zenu)'.[93]

---

[92] Hadithi imenukuliwa na imamu Bukhary na Muslim.
[93] Hadithi imenukuliwa na imamu Bukhary.

3-amtembelee endapo ataumwa na amuombee dua.
kutokana na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani -:
(Haki za Muislamu kwa Muislamu mwezake ni tano: kumsalimia, Kumtembelea anapo umwa, Kusindikiza jeneza lake, Kuitikia wito na mwaliko wake, Kumuombea dua pindi akitoa chafya) [94]

4- Ahudhurie mazishi yake pindi atapokufa. Kama ilivyo kwenye hadithi ya mtume iliyo tangulia hapo juu.

5- Akubali kiapo chake pale anapo muapia kwa lolote lile , na asifanye kinyume na alivyo apa. Kwa Hadithi iliyo pokewa na Albaraa bin Azib:
(Mjumbe wa Allah, - Allah amshushie rehema na amani- ametuamuru: Kumtembelea mgonjwa, kusindika jeneza lake, kumuombea dua aliye kwenda chafya, kumfanyia wema aliyeapa, kumnusuru aliyedhulumiwa, kuitikia wito (mwaliko) na kutoa salamu.)[95]

---

[94] Hadithi imenukuliwa na Bukhary na Muslim
[95] Hadithiimenukuliwa na imamu Bukhary.

6- kumpa nasaha pindi atakapo taka nasaha (ushauri) katika jambo lolote, kwa kumwelekeza lenye manufaa.
Kutokana na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:
" Pindi mmoja wenu akitaka nasaha kwa ndugu yake, ampe nasaha.[96]"

7- Apende ndugu yake apate kile anachopenda yeye akipate, na achukie kupatwa na kile anacho chukia yeye kupatwa nacho.
Kutokana na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:
" Hatakuwa mkamilifu wa Imani mmoja wenu hadi ampendelee ndugu yake (apate) kile anachokipenda yeye.[97].

8- Amnusuru na asimdhalilishe katika jambo lolote alilotaka kunusuriwa na kuungwa mkono.
Kutokana na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:
"Mnusuru ndugu yako aliye dhalimu au aliye dhulumiwa. Akaulizwa Mtume kuhusu namna ya kumnusuru anaye dhulumu akasema:

---

[96] Hadithiimenukuliwa na imamu Bukhary.
[97] Hadithiimenukuliwa na imamu Muslim.

Unachukua kilicho mkononi mwake, au unamzuia kudhulumu, na kumzuia kufanya kitendo chake, huko ndiko kumnusuru kwake.[98]
Na kauli yake mtume- Allah amshushie rehema na amani-: (Mwenye kurudisha heshima ya ndugu yake, Allah ataurudisha (ataulinda) uso wake na moto Siku ya Kiama.

9- Asimguse kwa ubaya au kumsababishia jambo asilo lipenda.
Kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:
Kila Muislamu kwa Muislamu mwenzake ni haramu; damu yake,mali yake na heshima yake.[99]
Na kauli yake: (Si halali kwa Muislamu yoyote kumtisha Muislamu mwenzake. Imenukuliwa na Imamu Ahmad na Abudaudi.
Na kauli yake: (Muislamu, ni Yule ambae Waislamu watasalimika kutokana na mdomo wake na mkono wake) .

10- Awe mnyenyekevu kwake asiwe na kiburi kwake, na asimuinue katika kikazi alichokaa

[98] Hadithi imenukuliwa na Bukhary na Muslim
[99] Hadithiimenukuliwa na imamu Muslim.

ambacho anastahiki yeye kukaa hapo, kwa kauli ya Allah: (Na usigeuze sura yako kwa kudharau watu (unapozungumza nao) na usitembee kwa kujivuna, hakika Allah hampendi kila aliye na kiburu mwenye majivuno mno).
Na kwa kauli yake Mtume - Allah amshushie rehema na amani:
"Hatonyenyekea yoyote kati yenu kwa ajili ya Allah isipokuwa Allah Mtukufu atampandisha daraja"

Pia kwa kile kinacho julikana kwa Mtume - Allaha amshushie rehema na amani-, kuwa alikuwa myenyekevu kwa kila mtu, na hamgombezi mtu wala haoni udhalili kwake kutembea akiwa amefuatana na mjane na masikini na anawatekelezea mahitaji yao.
Na kauli yake Mtume: (Asimsimamishe mmoja wenu mtu sehemu yake kisha akakaa yeye sehemu hiyo. Lakini tanueni na toeni nafasi.[100]

11- Hatakiwi kumhama (kutomzungumzisha) kwa zaidi ya siku tatu, kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:

[100] Hadithiimenukuliwa na imamu Muslim.

“Si halali kwa Muisilamu yoyote kumhama ndugu yake kwa zaidi ya siku tatu. Wanakutana huyu anamdharau huyu na huyu anamdharau mwingine. Na mbora wao ni Yule anayeanza kumsalimia mwenzake’.

12- Asimsengenye au kumpuuza, au kumdharau, au kumpa jina baya au kumletea maneno ya uzushi ili kumuharibu, kwa kauli ya Allah:
(Enyi mlio amini , jepusheni sana na dhana, hakika baadhi ya dhana ni madhambi, na msipe kuane, na mmoja wenu asimsengenye mwenzake, hivi anapenda mmoja wenu kula nyama ya ndugu yake akiwa maiti?, basi hamlipendi hilo…)[101]

Na kauli yake Allah: (Enyi ambao mlio amini waanaume wasiwadharau wanaume wenzao, na wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao, huenda hao wakakawa bora kuliko wao, na msiziaibishe nafsi zenu, na msipeane majina ya kejeli, ni uovu kutumia jina baya baada ya

[101] Sura Al hujraat (49) Aya ya 12

kuwa sasa ni Waumini, na asiyetubu basi hao ndio wadhalimu hasa.)[102]

Na Kauli yake Mtume - Allah amshushie rehema na amani:

(Hivi mnajua nini maana ya kusengenya? Wakasema: Allah na Mtume wake wanajua zaidi. akasema: ni kumtaja ndugu kwa jambo ambalo analichukia, wakasema: ikiwa ni kweli analo hilo ninalo lisema? Akasema Mtume: ikiwa hicho unachokisema ni kweli, basi umemsengenya, na ikiwa unayosema si kweli, basi umemzulia.) [103]

Na kauli yake Mtume Allah amshushie rehema na amani katika Hija ya kuaga: "Hakika damu zenu, mali zenu na heshima zenu kwenu ni haramu.[104]

Na kauli yake Mtume: "Hataingia peponi mtu mchochozi ".

13- Asimtusi sawa yuko hai au amekufa.

kwa kauli yake Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:

---

[102] Sura Al hujraat (49) Aya ya 11

[103] Hadithi imenukuliwa na imamu Muslim

[104] Hadithi imenukuliwa na imamu Muslim

(Kumtukana Muislamu ni uovu na kupambana naye ni ukafiri).
Na kauli yake: (Msiwatukane maiti, kwani wao wamefika katika yale waliyo yatanguliza).

14- Na asimfanyie husuda au kumdhania vibaya au kumbughudhi au kumchunguza.
kutokana na kauli ya Allah: (Enyi mlio amini , jiepusheni sana na dhana, hakika baadhi ya dhana ni madhambi, na msipekuane na mmoja wenu asimsengenye mwenzake,..[105]

15- Na asimfanyie ghishi na hadaa, au kumfanyia hiyana.
kutokana na kauli ya Allah:
(Na wale wanao waudhi Waumini wanaume na Waumini wanawake kwa mambo wasiyo yafanya, kwa hakika wamebeba uongo na dhambi za wazi mno)[106]
Na kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:
(Mambo manne yakipatikana kwa mtu, atakuwa mnafiki halisi, na atakayekuwa na sehemu ya tabia hizo anakuwa na sehemu ya unafiki hadi

---

[105] Sura Al hujraat (49) Aya ya 12
[106] Sura Al ahzaab (33) Aya 58.

atakapoacha: Anapoaminiwa hufanya hiana (hatekelezi amana), anapo hadithia huongopa, anapo ahidi hatekelezi ahadi, na anapogombana hufanya uovu.[107]

16- Aamiliane naye kwa tabia nzuri, ampe mazuri na kumuondolea maudhi na kero, anapokutana naye amuoneshe bashasha, akubali ihsani kutoka kwake na kusamehe kosa alilo mtendea, na asimbebeshe jambo asilo liweza. kwa kauli yake Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:
(Mche Allah popote ulipo,na baya lifuatilizie kwa jema, na wafanyie watu katika tabia nzuri).

17- Kumheshumu kama atakuwa mtu mkubwa kwake, kumfanyia upole kama atakuwa mtoto mdogo kwa kauli ya Mtume:
"Si miongoni mwetu Yule asiyeheshimu mkubwa wetu, na kumhurumia mdogo wetu. "

[107] Hadithi imenukuliwa na Muslim

# ADABU ZA KUZICHUNGA KWA WASIO WAISLAMU:

Muislamu anatakiwa kuamini kuwa mila zote na dini zisizo kuwa Uislam ni batili, na wafuasi wake ni makafiri, uislam ndio dini ya haki, na wafuasi wake hao ndio Waumini Waislamu, kwa kauli yake Allah: (Hakika ya dini ya kweli ni Uislamu..[108]...

Na kauli yake pia:

(Na yeyote atakae chagua dini isio kuwa Uislamu, hatakubaliwa kwake chochote (katika matendo yake mema) na akhera atakuwa miongoni mwa wenye kupata hasara) .

Na hapa basi Muislamu anatakiwa kuona kuwa yoyote asiyekuwa Muislamu ni kafiri.

Na ajilazimu kwa upande wake kwa mambo yafuatayo:

1- Kutokiri ukafiri wake , na kutoridhika naye sababu kuridhia ukafiri ni kufuru.

2- Kumchukia kama ambavyo Allah alivyomchukia, kwa vile Allah amemchukia, basi na Muislam pia yapasa amchukie.

---

[108] Sura Aali imran (3) Ata ya 19

3- Kutompenda mapenzi ya hali ya juu.
kwa kauli yake Allah: (Muumini asimfanye kafiri kuwa kipenzi wa kumnusuru.) [109]
Na kwa kauli yake pia: (Hauta waona watu wanao muamini Allah na kuamini Siku ya mwisho, wakiwa na mapenzi na wale wanao mpinga Allah na Mtume wake, hata wawe baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao…)

4- Kumfanyia usawa na uadilifu, na kumpatia kheri, endapo hakuwa mwenye kuupiga vita Uislamu, kwa kauli yake Allah:
(Allah ajawakatazeni kuhusiana na wale ambao hawaja pambana nanyi kwa ajili ya dini yenu, na hawaja kutoeni kwenye Nyumba zenu, kuwafanyia wema na kuwafanyia uadilifu, hakika Allah anapenda wafanyao uadilifu.[110]

5- Amhurumie huruma ya ujumla, kama kumpa chakula akiwa ana njaa, kumpa maji kama atapata kiu, kumpatia dawa kama ataumwa au kumuokoa kutoka katika jambo litakalo muangamiza, na kumuondolea kero.

---

[109] Sura Aali imran (3) Ata ya 19

[110] Sura Al mumtahina (60) Aya ya 8.

Kwa kauli ya Mtume - Allah amshushie rehema na amani: (Muhurumie aliye ardhini, atakuhurumia aliye mbinguni).[111]
6-Kutomuudhi katika mali yake na heshima yake, kama atakuwa si mwenye kuupiga vita Uislamu.
kwa kauli yake Mtume - Allah amshushie rehema na amani-: (Anasema Allah Mtukufu: "Enyi waja wangu, hakika mimi mwenyewe nimeji haramishia dhulma, na nimeifanya dhulma kati yenu pia kuwa ni haramu, hivyo msidhulumiane".

7- Inafaa kumpatia zawadi pia kukubali zawadi kutoka kwake, na kula chakula chake kama atakuwa miongoni mwa watu wa kitabu: awe Myahudi au mnaswara kwa kauli yake Allah:

(Leo mmehalalishiwa vilivyo vizuri, Na chakula cha walio pewa Kitabu ni halali kwenu na chakula chenu ni halali kwao...)[112]
Na imepokewa kuwa Mtume - Allah amshushie rehema na amani-, alikuwa ana alikwa chakula kwa Myahudi katika mji wa Madinah na

[111] Hatdithi imenukuliwa na Tabrany na Hakim
[112] Sura Al maida (4) Aya ya 5.

anahudhuria, na anakula kile alicho letewa katika vyakula vyao.

8- Kuto muozesha mwanamke wa Kiislamu,na inafaa kuoa mwanamke kutoka kwa watu wa kitabu kwa kauli yake Allah: (Na msiwaozeshe Washirikina hadi waamini…)[113]
Na kwa kauli yake katika kuhalalisha kuwaoa wanawake wa Watu wa kitabu:
(..Na (mmehalalishiwa kuwaoa) wanawake wema miongoni mwa waumini , na wanawake wema katika waliopewa Kitabu kabla yenu mtakapo wapa malipo (mahari) yao, mkikusudia kujihifadhi (na) sio wenye kukusudia uzinzi wala kuwa weka (wanawake hao) kinyumba ).

9- Asianze kumsalimia, na endapo yeye atamsalimia, basi amjibu kwa kusema: wa Alaykum, (na kwako pia).
Kwa kauli yake Mtume Allah, - Allah amshushie rehema na amani-: (Endapo watawasalimia Watu wa kitabu basi semeni: Wa alaykum, (na juu yenu) [114]

---

[113] Sura Al baqra (2) Aya ya 221.
[114] Hadithi imenukuliwa na Imammu Bukhary na Muslim

10- Kutojifananisha nao.
kwa kauli yake Mtume - Allah amshushie rehema na amani-:

"Atakajifananisha na watu basi atakuwa miongoni mwao[115]"

## ADABU NA WANYAMA:

Muislam anazingatia kuwa wanyama wengi ni viumbe wa kuheshimiwa,hivyo huwahurumia na kuzingatia adabu zifuatazo:
1- Kuwalisha na kuwanywesha wakiwa na njaa au kiu, kwa ushahidi wa maneno ya mtume wa Allah: (Katika kila aliye na ini bichi, kuna malipo)[116]

2- Kuwahurumia na kuwa wapole kwao: anasema mtume wa Allah: (nani aliye muhuzunisha huyu kwa watoto wake, mrejesheeni watoto wake). [117] Alisema haya, pale alipo muona Ndege anazunguka angani

---

115 Hadithi imenukuliwa na Imammu Bukhary na Muslim
116 Imepokewa na Imam Ahmad na Ibn Maajah.
117 Hadithi imepokewa na Abu Daudi.

akilia akitafuta makinda yake, ambao walichukuliwa na mmoja wa maswahaba wakiwa tunduni.

3- Kuto muadhibu wakati wa kumchinja au kumuuwa, kwa ushahidi wa maneno ya mtume wa Allah: (hakika mwenyezi Mungu ameandika wema kwa kila kitu, wakati wakuuwa fanyeni wema, wakati wa kuchinja fanyeni wema, na mmoja wenu akipumzishe kichinjwa chake, na anoe vizuri kisu chake).[118]

4- Mnyama asiadhibiwe wakati wa kumchinja kwa adhabu ya aina yoyote ile, kwa kumuacha na njaa, au kumpiga, kumbebesha mzigo mzito, au kumkata kata vipande kabla ya kumchinja, au kumchoma kwa moto, kwa ushahidi wa maneno ya mtume wa Allah amesema: (ameingizwa mwamamke mmoja motoni kwa sababu ya Paka, aliye mfungia mpaka akafa, akaingia kwa sababu hiyo motoni, hakumpa chakula wala kinywaji, na wala hakumuachia ale vidudu vya Ardhini). [119] imepokewa Na Bukahri.

[118] Imepokewa na Imam Muslim.
[119] Imepokewa na Abu Daudi.

Na alipita mtume sehemu ambapo palikuwa na sisimizi, walio chomwa moto, akasema (hakika hapasi kuadhibu kwa moto, isipokuwa mola mlezi wa moto).

5- Ni halali kuwauwa wanyama wenye maudhi, kama vile mbwa mwenye kujeruhi watu, na mbwa mwitu, Nyoka, Panya, na Nge au mfano wao.
Anasema Mtume wa Allah: (aina tano za wanyama wabaya wauwawe Haram tukufu au nje : Nyoka, Kunguru, mbwa mwenye kungata watu, na Hid-a (kipanga). [120] Kama ilivyo halalishwa pia kuuwa Nge.

6- Pia inafaa kumwekea Mnyama alama sikioni likihitajika hilo, mtume ameonekana akimweka alama Ngamia wa sadaka kwa mkono wake mtukufu, ama wasio wanyama hoho (ambao ni Ng'ombe, mbuzi, kondoo na Ngamia), kama vile punda haifai kuwawekea alama usoni, Anasema Mtume wa Allah pale alipo muona Punda amewekwa Alama usoni: (Amemlaani Allah

---

[120] Imepokewa na muslim.

aliye muweka Alama Huyu usoni)[121] Imepokewa na Muslim.

7- Kujua haki za Allah kwa wanyama, kwa kuwatolea zaka ikiwa ni katika wanyama wa kutolewa zaka.

8- Kutopumbazwa nao, kwa kucheza nao mpaka kufikia kusahau kumkumbuka Allah.
Anasema Allah Mtukufu: (Enyi mlio amini msipumbazike kwa mali zenu wala watoto wenu mka acha kumtaja Allah).

Hizi ni adabu kadhaa ambazo Muislamu inapasa azichunge kwa wanyama, kwa kumtii Allah na Mtume wake, na kufuata amri ya sharia ya uislam, sharia yenye huruma, sharia yenye kheri kwa viumbe wote binadamu na wanyama.

---

[121] Imepokewa na muslim

# KUHUSU SHERIA NA ADABU ZA KUCHUNGA KWENYE KUKAA NA KIKAZI:

Maisha yote ya Muislamu yapo chini ya mwenendo wa Kiislamu, ambao unahusika na kila kipengele cha maisha, hata kukaa kwa Muislamu na jinsi anavyokaa na ndugu zake.
Hivyo yampasa muislam afuate Adabu zifuatazo wakati wa kukaa kwenye kikazi:

1- kabla ya kukaa, awasalimie watu waliopo kwenye kikazi hicho, kisha ndio akae, wala asimnyanyue mtu yeyote aliye kaa kutoka mahali pake, wala hakai baina ya watu wawili bila ya idhini yao, kama Amesemavyo Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam): (Asimyanyue yeyote miongoni mwenu mtu kutoka kwenye kikazi chake kisha akae yeye, lakini panueni au peaneni nafasi).[122] Na alikuwa Ibn Umar akisimama mtu yeyote kwa ajili yake kutoka kwenye kiti chake, hakai hapo

[122] [Muslim na Bukhari]

aliposimama, kufuatia maneno ya Mtume, swalallahu alayhi wa sallam, alisema: "Haijuzu kwa mtu kuwatenganisha watu wawili bila ya idhini yao. "[123]

2- Iwapo mtu atasimama kutoka kwenye kiti chake kisha akakirudia, ana haki zaidi yeye ya kukaa, kwa sababu amesema Mtume (Swalla Allaahu, alayhi wa aalihi wa sallam): ((Akiinuka mmoja wenu kutoka katika kiti, na akarudi kwenye kiti hicho,basi yeye anayo haki zaidi ya kukaa hapo)).[124]

3- Asikae katikati ya kikazi mduara, kwa sababu Hudhaifah amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa alayhi wa sallam) (Amelaaniwa anayekaa katikati ya kikazi mduara) Imepokewa na Abu Daud.

4- Na miongoni mwa adabu ambazo ni lazima azizingatie akiwa kwenye kikazi, ni:
kutochokoa meno yake, kutoingiza mkono wake puani, kukwepa kutema mate, na achague

---

[123] Imepokewa na Abu Daawuud na Al-Tirmidhiy.
[124] Imesimuliwa na Muslim.

maneno mazuri wakati wa kuzungumza.Na mtu mwingine akimsemesha amsikilize na anyamaze, na asimkatishe.
Muislamu anapo shikamana na adabu hizi hushikamana nazo kwa sababu mbili:
Kwanza: Ili asiwadhuru ndugu zake kwa kauli au vitendo vyake, kwa sababu kumdhuru Muislamu ni haramu: "Muislamu ni yule ambaye wako salama waislam wenzake kutokana na ulimi wake na mikono wake "
Na ya pili: kwamba analeta upendo na mapatano kwa ndugu zake. Kwa vile sheria imeamrisha urafiki na maelewano baina ya Waislamu.
Ikiwa anataka kukaa barabarani, anapaswa kuzingatia adabu zifuatayo:

1- Kuinamisha macho yake, na ayazuie kumwangalia yeyote katika wanawake, wala asimhusudu yeyote kwa macho yake, wala kumdharau.

2- Ajizuie na kuwaudhi wapita njia, kwa aina yeyote ya maudhi, kwa ulimi wake, asiwatukane, asiwashutumu, asiwa aibishe na kuwatia kasoro, na kwa mkono wake asiwapige wala kuwadhuru

na kuwayang'anya mali zao, wala asiwazuie na kuwabana wapita njia wengine.

3- Kumrudishia salamu kila aliye msalimia katika wapita njia, kwani kurudisha salamu ni wajibu, kwa kauli yake Mola Mtukufu: (Na mkiamkiwa kwa maamkio, basi toeni salamu iliyo bora zaidi au irudisheni) .

4- Kuamrisha jambo jema lililo achwa mbele yake, na lililo puuzwa hali ya kuwa analiona, kwani yeye ndiye mwenye wajibu katika hali hii ya kuamrisha, kwa sababu kuamrisha mema ni wajibu kwa kila Muislamu. Na mfano wake: Iwapo mwito wa kusali (Adhana) , na watu wa mkusanyiko au mtu yeyote njiani asiitikie, basi ni lazima awa amrishe waende kuswali.

5- Kukataza maovu anayo yaona mbele yake, kwani kukataza maovu ni wajibu, kama ilivyo kuamrisha mema, kwa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) Atakaye uona uovu miongoni mwenu, na aubadilishe (Auondoe). Katika hali hii, ni lazima aondoe ovu likiwa lipo ndani ya mipaka ya uwezo wake.

6- Kumwelekeza aliye potea njia akimtaka msaada.

Na adabu zote hizi ni kwa kauli yake Mtume wa Allah - amani iwe juu yake -, (Tahadharini na kukaa njiani. Wakasema: Hatuna khiari. Ni mikusanyiko yetu humo, na tunazungumza humo." Akasema: "Basi mkikataa isipokuwa mkusanyike, basi ipeni njia haki yake." Wakasema: "Ni ipi hiyo haki ya njia? . akasema: kuamrisha mema na kukataza maovu." Na katika baadhi ya mapokezi kuna nyongeza: "Na kuwaongoza walio potea)..

Na Miongoni mwa adabu za kukaa ni kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha anapo inuka kutoka kwenye kikazi, kama kafara ya yale aliyo yapata katika kikazi, kwani Mtume wa Allah- alikuwa akisema: Ikiwa akitaka kuinuka kutoka kwenye kikazi husema: (Umetakasika ewe Mwenyezi Mungu, na sifa njema zote ni zako. Nashuhudia ya kwamba hapana mungu apasae kuabudiwa kwa haki Isipokuwa wewe, nakuomba msamaha na ninatubia kwako." Aliu lizwa kuhusu hilo na akasema: "Ni kafara kwa yale yanayopatikana katika mkusanyiko."[125]

---

[125] Imepokewa na Al-Tirmidhiy.

# SHERIA ZA KULA NA KUNYWA:

Mwislamu huona chakula na vinywaji kama njia ya kumfikisha kwenye lengo maalum, na wala sio ndio lengo lenyewe. Kwa hivyo Mwislam hula na kunywa kwa lengo la kulinda afya ya mwili wake ambao ndio humwezesha kufanya Ibada, hii ibada ndio ambayo humpa hadhi ya kupata utukufu na furaha kesho Akhera, kwa hivyo Mwislam Hali na kunywa kwa lengo la kushiba na matamanio.

Na kwa hivyo Muislamu anashikamana na adabu maalum za kisheria katika kula na kunywa kwake, ikiwa ni pamoja na:

## a. Adabu kabla ya kula, ambazo ni:

1- Kuhakikisha kuwa chakula chake na kinywaji chake kinatokana na chumo la halali, kisicho na uchafu wa haramu wowote ule, Mwenyezi Mungu amesema: "Enyi mlio amini kuleni katika vitu vizuri tulivyo kuruzukuni".

Na kwa kauli yake, swalah na salamu za Mwenyezi Mungu zimshukie: (Kila kinacho ota kutokana na haramu, basi moto ni sahihi zaidi kwake).

2- Kwamba yawe makusudio na nia yake katika kula na kunywa kwake ni kumuabudu Allah,katika ucha mungu, ili apate thawabu kwa kula na kunywa kwake. Jambo lililohalalishwa kulifanya huwa ni ibada, na analipwa kwa kulitenda, iwapo mtu atakuwa na nia mzuri wakati analitenda.

3- Kuosha mikono yake kabla ya kula ikiwa kuna uchafu ndani yake, au ikiwa hana yakini kuwa ni safi.

4- Kukaa kwa staha kama alivyokuwa akikaa Mtume, na kwa kauli yake: (Sili kwa kuegemea, lakini mimi ni mtumwa ninaye kula kama alavyo mja, na nina kaa kama mja akaavyo). [126]

5-Kutosheka na kile kinacho patikana katika chakula, na sio kukitia dosari, akipenda akile, na ikiwa hakipendi akiache, kwa hadithi ya Abu Hurairah. Allah awe radhi naye: (Mtume wa Mwenyezi Mungu na amani ziwe juu yake, hakuwahi kukikashifu chakula, akipenda hukila, na akikichukia alikiacha) Imepokewa na Al-Bukhari.

[126] Imepokewa na Al-Bukhari.

6- Kula kwa pamoja na wengine, awe mgeni, familia, mwana au mtumishi, kwa sababu ya Hadithi: "Kusanyeni chakula chenu, na mtajeni jina la Mwenyezi Mungu juu yake, naye atakubarikini humo."[127]

## b. Adabu ya kula wakati wa kula:

1- Kwanza kuanza kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa sababu mtume amesema: (Akila mmoja wenu, na alitaje jina la Mwenyezi Mungu, na akisahau kutaja jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu mwanzoni, na aseme: Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwanzo na mwisho wake)).[128]

2- Kumhimidi Mwenyezi Mungu baada ya kula na kunywa, kwa sababu Mtume amesema: "Mwenyezi Mungu ameridhika na mja anae kula chakula na kumhimidi kwacho, au ana kunywa kinywaji na kumhimidi. kwa ajili yake."[129]

---

[127] Imepokewa na Abu. Daawuud na Al-Tirmidhiy

[128] Imepokewa na Abu Dawood na Al-Tirmidhiy.

[129] Imesimuliwa na Muslim.

3- Kula kwa mkono wake wa kulia, na kufanya tonge liwe dogo na kutafuna vizuri, na kula kilicho karibu yake, si kula katikati ya sahani, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam: (Ewe kijana, mtaje Mwenyezi Mungu na kula kwa mkono wako wa kulia na kila kilicho karibu nawe).

4- Kikimdondoka kitu chochote katika chakula basi akiokote, na atoe uchafu kisha ale, kama alivyosema mtume rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: (Likianguka tonge la mmoja wenu, basi alichukue, aliondoe. madhara yake na kuleni, wala msimwachie shetani).[130]

5- Kutopuliza chakula cha moto, asubiri kipoe ndio akile, kwa mujibu wa Hadithi ya Ibn Abbas Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, Mtume Rehema na amani ziwe juu yake. , "amekataza kupumua ndani ya sahani (ya chakula) au kupuliza ndani yake."[131]

---

130 Imesimuliwa na Muslim

131 Imepokewa na Al-Tirmidhi

6- Kujiepusha na kushiba kupita kiasi, kama alivyosema Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam): (Mwanadamu hajapata kujaza chombo kibaya kuliko tumbo lake, inamtosha mtu matonge machache ambayo yatausimamisha mgongo wake, Asipofanya hivyo, basi theluthi moja iwe ni ya chakula chake, theluthi moja iwe ni ya kinywaji chake, na theluthi moja iwe kwa ajili ya pumzi yake))

7-Kwamba asianze kula wala kunywa, na katika baraza kuna aliye bora zaidi yake, kwa utu uzima wake, au mtu mwenye kumzidi kwa fadhila, kwa sababu hilo linaenda kinyume na tabia njema.

8- Kutowatazama na kuwachunguza wenzake anao kula nao wakati wa kula, kwani hilo linawafanya waone haya.

9- Asifanye yale ambayo watu huwa kawaida huyaona ni kinyaa, asikungutie mkono wake kwenye sahani, au kuinamia kwenye sahani wakati wa kula, kisije kikaanguka kitu kinywani mwake, pia mfano akikata kipande cha mkate kwa meno yake,basi asikirudishe tena kwenye

sahani, pia asizungumze maneno ya kuwaudhi wenzake wakati wa kula.

## MAADILI YA KUSAFIRI:

Kusafiri ni moja ya mahitaji ya dharura katika maisha, hivyo h Hajj na Umra, kutafuta elimu na riziki, na kutembelea ndugu, hayo yote lazima mtu asafiri. Kwa hivyo, Uislamu unajali sana safari, na kuiwekea maadili na hukumu na adabu zake, na Muislamu mwema lazima ajifunze na kutekeleza haya maadili ya safari, ambayo ni:

1- Kufupisha Swalah ya rakaa nne, kwa kuiswali rakaa mbili tu, isipokuwa Maghrib, kwani anaswali tatu,
Na mda wa kuanza kufupisha , au kupunguza swala ni tokea anavyo toka katika anaoishi, amesema Allah Mtukufu " na pindi mtakapo safiri basi hamna ubaya kwenu kupunguza swala" [132]
Na kwa maneno ya Anas: tulitoka na Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa

[132] Al Nisaa 101.

aalihi wa sallam) katiaka safari kutoka Madina hadi Makka. , na alikuwa akiswali swala za rakaa nne rakaa mbili, mpaka tukarudi Madina." Imepokewa na al-Nasa'i na al-Tirmidhiy.

2-Kujuzu kupaka juu ya viatu (khof) mda wa siku tatu mchana na usiku, kwa kauli ya Ali (Radhiya Allaahu 'anhu) amesema: (((Ametujaalia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwa msafiri, siku tatu mchana na usiku, na mchana mmoja na usiku mmoja kwa mkazi wa mji, maana yake ni kupaka juu ya viatu aina ya Khofu)) [133]

3- Kuruhusiwa kutayammam, ikiwa maji yamepotea au ni vigumu kupatikana au bei yake imepanda. kwa sababu ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na mkiwa wagonjwa au mko safarini au mmoja wenu akajisaidia haja kubwa, au mkiwagusa wanawake. na hamkupata maji, basi mtayammam kwa mchanga safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu).[134]

---

[133] Imepokewa na Ahmad, Muslim, al-Nasa'i na Ibn Majah.

[134] Al-Nisaa: 43.

4- Kuruhusiwa kufuturu (kutofunga) kwa msafiri, kwa kauli yake Mola Mtukufu isemayo: (Mwenye kuwa mgonjwa miongoni mwenu au yumo safarini basi na atimize siku alizofungua kwa kuzilipa baadae)' [135].

5- Kuruhusiwa kuswali swala ya Sunna juu ya mnyama au kipandwa popote anapoelekea, hata kama sio kibla, kwa kauli ya Ibn Umar – Allah amridhie - amesema kuwa: Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alikuwa akiswali swala yake ya Sunna juu ya Mnyama. Popote alipo elekea ngamia wake)) [136]

6- Ni Ruhusa kuunganisha Adhuhuri na Alasiri, na vilevile kuunganisha Maghrib na Isha, kwa kuziswali pamoja kwa kuzitanguliza, kwa kuswali Adhuhuri na Alasiri wakati wa Adhuhuri, na Magharibi na Isha wakati wa Magharibi, au kwa kuchelewesha. kuswali Dhuhr na Alasiri wakati wa Asr, na Maghrib na Isha wakati wa Isha. Kwani Muadh (radhi za Allah ziwe juu yake) amesema: (Tulitoka pamoja na Mtume

---

[135] Al-Baqarah: 184,

[136] Imepokewa na Bukharin a Muslim

(Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam) katika vita vya Tabuk, na alikuwa akiswali Swalah ya Adhuhuri na Alasiri, na Sala za Maghrib na Isha kwa pamoja).[137]

Ama Kuhusu adabu,ni:
1-masurufu yake ya safari yawe ni ya halali, na aache matunzo ya mke, wana na mzazi ambaye inamlazimu kumhudumia.

2- Kuagana na jamaa zake, ndugu zake na marafiki zake, na kuomba dua hii: Ninaikabidhi Dini yenu kwa Allah, na amana yenu, na mwisho wa matendo yenu, na watamuambia wale wano muaga: Mwenyezi Mungu akupe ucha mungu. na akakusamehe madhambi yako na akakuelekeza kwenye kheri, popote unapo elekea, kama ulivyoelekea kwenye maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam): (Hakika Luqman alisema: Ikiwa kitu kimekabidhiwa kwa Mwenyezi Mungu akihifadhi, basi hukihifadhi)[138]

137 Imepokewa na Bukharin a Muslim
138 Imepokewa na Annasai

Alikuwa akiwaambia wanaomuaga: "Mimi naikabidhi kwa Mwenyezi Mungu Dini yenu, amana yenu, na hitimisho la matendo yenu." [139]

3- Kwamba wasafiri wamchague mmoja wao kuwa kiongozi wao, anaye waongozi kwa kuwashauri, kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: (Wakitoka watatu safarini, basi wamfanye mmoja wao kuwa kiongozi wao).

4- Atoke safarini pamoja na watu watatu, wanne au zaidi, baada ya kuwachagua wanaostahiki kusafiri pamoja naye, kwa sababu ya kauli ya Mtume aliyosema: "Msafiri peke yake ni shetani, na wasafiri wawili ni mashetani wawili, na watatu ndio wasafir." [140]
Na kwa kauli yake pia: "Lau watu wangelijua ninayo yajua mimi (madhara) yatokanayo na kusafiri mtu peke yake, asingesafiri mtu peke yake usiku mmoja." [141]

5-Kuswali swala ya istikhara kabla ya safari yake, kama alivyohimiza mtume hilo, mpaka

---

[139] Imepokewa na Abu Daud.
[140] Imepokewa na Abu Daud, al-Nasa'i na al-Tirmidhiy
[141] Imepokewa na Al-Bukhari.

Mtume - swala na salamu za Allah zimshukie – alikuwa akiwafundisha mswahaba wake hiyo swala ya Istikhhra kama anavyo wafundisha Sura katika Qur-ani, na katika mambo yote))[142]
6- Aseme anapopanda kwenye usafiri wowote ule: Bismillahi, Allahu Akbaru, Allahu Akbaru, Subhana lladhi sakhara lana hadhaa wamaa kunaa lahu Muqriniyna, wa inaa ilaa rabbinaa lamunqalibuuna, (Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu ni mkubwa, Mungu ni mkubwa, Mungu ni mkuu, Ametakasika aliyetufanyia mzaha haya na hatukufungana nayo, na kwa Mola wetu Mlezi tutamtukana) . Allahuma inii as'aluka fiy safarinaa hadha albirra wa taqwaa, wamina al amali maa tardhwa, Allahumaa hawwin alaynaa safarinaa hadha, watwi anaa buudahu, Allahuma inii audhu bika min waathaai al safari wa kaabati almandhari, wasuua almunqalabi fiy lmali wal ahli
(Ewe mola, mimi nakuomba katika safari yetu hii, utupe ucha mungu, na utujaalie tufanye yale unayo yaridhia, Ewe mola, ifanye iwe nyepesi kwetu hii safari, na ukunje umbali wake iwe mfupi, ewe Mola, wewe upo nasi katika

[142] Imepokelewa na Al-Bukhari

safari, na mlinzi wa familia zetu tulio waacha, ewe Mungu, najikinga Kwako kutokana na tabu za safari, na marejeo mbaya kwenye mali na familia.

7- Asafiri siku ya Alhamisi, mapema mchana, kwa sababu Mtume, swallallahu alayhi wa sallam, amesema: “Ewe Mola, ubariki umma wangu katika kujihimu kwao.”

8- Kwamba aseme (allahu akbaru) kila anapopanda niinuko, kwa sababu Abu Huraira, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, alisema: Mtu mmoja alisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nataka kusafiri, niusie. Akamwambia: (kuwa mcha Mungu, na lete Tkbira kila kwenye muinuko).[143]

9- Iwapo anawaogopa watu wabaya kumdhuru basi aseme: (Ewe Mola wetu tumekuweka mbele yao, na tunajikinga kwako kutokana na shari zao) kwa sababu Mtume, swallallahu alayhi wa sallam, amesema hayo.

143 Imepokewa na Attirmidhiyi.

10- Kumuomba Allah katika safari yake kheri ya dunia na ya Akhera, kwani dua wakati wa safari hujibiwa, kama alivyosema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam): ((Dua tatu hujibiwa, hapana shaka juu ya hilo: dua ya mwenye kudhulumiwa, dua ya msafiri, na dua ya baba kwa mtoto wake)) [144].

11- Anaposhuka aseme: (audhu bikalimaati llahi taamaati min shari maa khalaqa), Najikinga kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyo kamili kutokana na shari ya alichokiumba.

12- Anapo fika katika mji aseme: Ewe Mola Mlezi wa mbingu saba na zinavyo funikwa na vivuli vyake,Mola Mlezi wa ardhi saba na vilivyo bebwa juu yake, Mola Mlezi wa mashetani na wanavyo vipoteza, Mola Mlezi wa pepo na vilivyo peperushwa na huo upepo, basi tunakuomba kheri ya kijiji hiki na kheri ya watu wake, na tunajikinga kwako na shari yake, na shari ya watu wake, na shari ya yaliyomo ndani yake) kwani Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Alikuwa akisema hivyo.

---

144 Imepokewa na Attirmidhiyi.

13- Akirejea kutoka katika safari yake, asome dua ya safari, na aongeze mwisho wake: (tumerejea, hali ya kutubu,na wenye kutakasa ibada kwa mola wetu mlezi, wenye kushukuru kwa neema zake.Ikitubu, waja wa Mola wetu Mlezi) kwa sababu yeye Mtume, swala na amani zimshukie. Alisema hivyo.

14- Asiingie kwenye familia yake usiku bila ya wao kujua, ili asije kuwashtukiza ghafla hali ya kuwa wao hawana maandalizi yoyote. kwani huu ulikuwa ni muongozo wa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam).

15- Kwamba asisafiri mwanamke ila pamoja na Mahram wake – kaka, au baba, nk. kwa sababu Mtume, swallallahu alayhi wa sallam, amesema: (Haijuzu kwa mwanamke anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kusafiri siku moja na usiku wake, isipokuwa akiwa na Mahram wake).

# ADABU YA MAVAZI:

Muislamu analazimika kuvaa kwa kufuata utamaduni na adabu zifuatazo:

1- Mwanaume asivae Hariri hata kidogo, iwe katika vazi au kilemba au kitu kingine chochote, kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: ((Mavazi ya Hariri na dhahabu yameharamishwa kwa wanaume wa Umma wangu, na wamehalalishiwa kwa wanawake wao)).[145]

2- Asirefushe nguo yake au suruali yake hadi chini ya vifundo vya miguu, kwa sababu Mtume, swallallahu alayhi wa sallam, amesema: "Kilicho chini ya vifundo vya miguu ni vya Motoni." [146]

3- Kwamba vazi jeupe linapendekezwa zaidi kuliko mavazi rangi nyengine, ingawa kuvaa vazi la rangi nyingine inafaa, kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: ((Vaeni nguo zenu nyeupe,

---

145 Al-Tirmidhiy: 1720.

146 Imepokewa na Al- Bukhari.

kwani ni miongoni mwa nguo zenu bora na wavalisheni sanda nyeupe maiti zenu.)).

4- Kwa mwanamke wa Kiislamu arefushe vazi lake mpaka afunike miguu yake, na ateremshe vazi lake juu ya lifunike kichwa chake, na kufunika shingo yake na kifua chake, kwa sababu ya kauli ya Allah Mtukufu: ((Ewe Mtume waambie wake zako na binti zako na wanawake wa Waumini wawateremshe –ziwe ndefu- nguo zao)[147]

5- Mwaume asivae pete ya dhahabu, kwa sababu Mtume, swallallahu alayhi wa sallam, amesema: ((Nguo za Hariri na dhahabu ni haramu kwa wanaume wa umma wangu na wamehalalishiwa wanawake wao)). Hakuna ubaya kuvaa pete ya fedha.

6- Asitembee na kiatu kimoja, kwa sababu amesema Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam): ((Asitembee mmoja wenu katika kiatu kimoja, Ima avivue vyote pamoja, au avae vyote viwili)) [148]

---

[147] Al-Ahzab: 59.

[148] Imepokewa na Muslim.

Na akivaa viatu anaanza na mguu wa kulia, na akivua anaanza na kushoto, kwa maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam): ((anapovaa viatu mmoja wenu aanze kulia, na akivua aanze kushoto)) [149]

Na vivyo hivyo katika kuvaa nguo zake kwa kauli ya Aisha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi: (( alikuwa mjumbe wa Allah _rehema za Allah ziwe juu yake na amani- anapendezewa na kuanza upande wa kulia, katika mambo yake yote, katika kuvaa viatu vyake, kuchana nywele, na katika kujitwaharisha."[150]

7- Kwamba mwanamume asivae nguo za kike, na wanawake wasivae nguo za kiume, kwa sababu Mtume, swallallahu alayhi wa sallam, amekataza hilo kwa kusema: ((Mtume wa Mwenyezi Mungu alimlaani mwanamume anayevaa nguo za kike. na mwanamke aliyevaa vazi la mwanamume))[151]

---

[149] Imepokewa na Muslim.

[150] Imepokewa na Muslim.

[151] Imepokewa na al-Nasa'i.

Kama pia mtume alivyowalaani wanaojifananisha na wanaume wanaojifananisha na wanawake.na wanawake wanaojifananisha na Wanaume)).[152]

8- Aseme akivaa nguo mpya au vazi jipya: ((Ewe Mola, sifa njema ni Zako. Wewe ndie uliye nivisha vazi hili. Nakuomba kheri yake na kheri ya iliyo tengenezwa, na Najikinga Kwako kutokana na shari yake na shari ya iliyo tengenezwa kwayo.))[153]

## ADABU ZA KIMAUMBILE:

Mambo yaliyothibiti ya Silika ya kimaumbile kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni matano, nayo ni haya katika kauli yake: ((mambo matano ni sehemu ya silika ya asili: kunyoa nywele za sehemu ya siri, tohara. , kukata masharubu, kung'oa mywele za kwapa, na kukata kucha)).
Na kukata sharubu zinazoning'inia juu ya mdomo ni Sunnah, ama ndevu hatakiwi kuzikata, kwa mujibu wa kauli ya Mtume

---

[152] Imepokewa na Al-Bukhari 1/280.
[153] Abu Daawuud na Al-Tirmidhiy.

(Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam): "Punguzeni sharubu na ziacheni ndevu ziwe ndefu." [154]
Na kauli yake: ((Tofautianeni na washirikina, kateni masharubu na ziacheni ndevu...))[155]
Ajiepushe kunyoa Qaza, ambayo ni kunyoa sehemu ya kichwa na kuacha sehemu yake, kwa mujibu wa Ibn Omar,- Mwenyezi Mungu amuwiye radhi: ((Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amekataza Qaza))[156] Imeafikiana.

Na muislamu akiacha nywele zake zikawa ndefu, basi azitunze vizuri, ziwe safi, na azichane vizuri, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam): ((Mwenye nywele ndefu basi azitunze vizuri))[157]
Muislamu azing'oe nywele zake za kwapa au azinyoe, na sifa mojawapo ya silika ya kimaumbile ni kupunguza kucha, na inapendeza kuanza kwa mkono wa kulia, kisha wa kushoto,

---

[154] Imepokewa na Muslim
[155] Imepokewa na Muslim.
[156] Imekubaliwa na Bukhari na Muslim
[157] Imekubaliwa na Bukhari na Muslim.

kisha mguu wa kulia, kisha wa kushoto. Na Muislamu anayafanya hayo yote kwa nia ya kuiga mfano wa Mtume (Swalla Allaahu ʽalayhi wa aalihi wa sallam) na kumfuata ili apate ujira wake, kwani vitendo ni kwa nia, na kila mtu atalipwa kwa mujibu wa nia yake.

## ADABU ZA KULALA:

Muislamu anauona usingizi kuwa ni miongoni mwa neema ambazo Mwenyezi Mungu amewaneemesha waja wake, katika kauli yake: ((Na amekufanyieni kutokana na rehema zake usiku na mchana, ili mtulie humo na kutafuta fadhila zake na mpate. shukuru) [158].
Miongoni mwa shukrani kwa neema hii Muislamu huzingatia adabu zifuatazo katika kulala kwake:

1- Asicheleweshe kulala baada ya Swalah ya Ishaa isipokuwa akiwa na dharura, mfano kuyarejea masomo yake, au akiwa na mazungumzo na mgeni, au kujumuika na watu,

[158] Al-Qasas74.

kama alivyosimulia Abu Barza kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‛alayhi wa aalihi wa sallam) alikuwa hapendi kulala. kabla ya sala ya Ishaa na mazungumzo baada yake).[159]
Alifanya hivyo akihofia kuchelewa kuswali swala ya Alfajri.

2- Ajitahidi asilale bila ya kutawadha, kwani Mtume (Swalla Allaahu ‛alayhi wa aalihi wa sallam) alimwambia Al-Baraa bin Azib radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: ((Ukilala tia udhuu wako kama unavyotia udhu wako wa swala.))[160]

3- Alale kwa ubavu wake wa kulia na alalie mkono wake wa kulia,  na hakuna ubaya kubadili upande wake wa kushoto baadae, kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema: ukifika mahali pako pa kulala, tawadha udhu wako wa swala, kisha lala ubavu wako wa kulia) na akasema: ((Ukilala na hali umetoharika, lalia Mkono wako wa kulia .)

---

159 Bukhari na Muslim.

160 Imekubaliwa na Bukhari na Muslim.

4- Asilalie tumbo lake, mchana au usiku, imepokewa kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema: (hakika kulala hivi (kulalia tumbo) hapendi Allah mtukufu)) .[161]

5- Asome dua zilizopokewa kadiri awezavyo, ikiwa ni pamoja na:
- Kusema: Subhana llah, na Alhamdulillahi, na Allahu akbaru, mara thelathini na tatu, akamilishe mara ya mia kwa kusema : Allahu akbaru. (Ametakasika Mwenyezi Mungu, sifa zote ni za Allah, Mwenyezi Mungu ni mkubwa) mara thelathini na tatu, kisha anasema: Mwenyezi Mungu ni mkubwa) kukamilisha mia, kwa sababu Mtume, swala na salamu zimshukie, alimwambia Ali na Fatima, Mwenyezi Mungu awawie radhi, pale walipomuomba mtume awapatie mtumishi: ((Je, nisikuambie kitu bora kuliko ulichoomba? Ukienda kulala kitanda kwako, basi mtukuze Mwenyezi Mungu mara thelathini na tatu, na mtakaseni Mwenyezi Mungu thelathini na tatu, na mtukuzeni Mwenyezi Mungu thelathini na nne, kwani

161 Imepokewa na Al-Tirmidhiy: 2768.

kufanya hivyo ni bora kwenu kuliko kupewa mtumishi ."[162]

- Kusoma Ayat al-Kursi, na Qul huwa llahu Ahadu, na sura mbili za Al muawadhatain,kama yalivyokuja mahimizo ya hilo.

- Kusema anapoamka: (Alhamdulillahi alladhi ahyana baada ma amatanaa wailayhi al nushuur) Asifiwe Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai baada ya kutufisha na kwake tutafufuliwa.

Wabillahi Tawfiq

Chanzo ni kitabu: Minhaj Al Muslim
Cha mwanazuoni Sheikh / Abi Bakr Al-Jazaery.
Pamoja na kuhaririwa kidogo.

162 Imepokewa na Muslim.

# YALIYOMO:

KUMUAMINI ALLAH: ............................................ 3
ADABU ZA KUZICHUNGA KWA ALLAH:....................11
KUWA NA ADABU KATIKA MANENO YA ALLAH ........17
KUCHUNGA ADABU PAMOJA NA MTUME- WA ALLAH ALLAH AMSHUSHIE REHEMA NA AMANI ..................20
ADABU KWA MSWAHABA NA WAUMINI:.................23
AMA KWA UPANDE WA MAIMAMU WA KIISLAMU MIONGONI MWA WASOMAJI QUR,ANI,WATU WA FANI YA HADITHI, WATU WA FIQIH NA WENGINEO, KWA HAKIKA NI KUWA:.......................................26
AMA VIONGOZI WENYE MAMLAKA:........................28
MUISLAMU NA NAFSI YAKE:..................................31
HAKI ZA WAZAZI WAWILI:....................................37
HAKI ZA WATOTO:...............................................40
HAKI ZA NDUGU: ...............................................42
HAKI ZA WANA NDOA:..........................................42
HAKI ZA MKE:.....................................................45

HAKI ZA MUME: .................................................47
ADABU PAMOJA NA NDUGU WA KARIBU: ...............50
KUCHUNGA ADABU ZA JIRANI:..............................52
ADABU ZA MUISLAMU NA HAKI ZAKE:....................55
ADABU ZA KUZICHUNGA KWA WASIO WAISLAMU:..65
ADABU NA WANYAMA:.........................................69
KUHUSU SHERIA NA ADABU ZA KUCHUNGA KWENYE KUKAA NA KIKAZI: ...............................................73
SHERIA ZA KULA NA KUNYWA:..............................78
MAADILI YA KUSAFIRI:........................................83
ADABU YA MAVAZI:.............................................92
ADABU ZA KIMAUMBILE:......................................95
ADABU ZA KULALA: .............................................97